ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nne – Tarehe 16 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

TAARIFA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuanza kikao chetu naomba nichukue fursa hii kuwakaribisha wageni ambao wako kwenye ukumbi wa juu. Wageni hawa ni Kamati ya Afya kutoka Jimbo la Muyuni jumla yao ni 18 wakiongozwa na Masheha wa Shehia zote tatu za Muyuni. Waheshimiwa Wajumbe, wageni hawa ni wa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wageni wetu karibuni sana. Kwa hivyo, wageni naomba musimame na muwasalimie Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Tunakushukuruni sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Abdalla Moh'd Ali (Kny: Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza Migogoro ya Ardhi. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 31

Baraza la Wawakilishi Kupeperusha Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi (Kny: Hija Hassan Hija) – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa tangu kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi Zanzibar tumekuwa tukipeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

a) Ni kwa nini Baraza la Wawakilishi inapeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bendera ya Zanzibar tu.

b) Kama hoja ni Baraza la Wawakilishi kutambulika ndani ya Katiba ya Tanzania kwa nini bendera ya Zanzibar isipeperushwe katika Afisi za Bunge.

c) Je, kama hivi ndivyo ni sahihi kusema kuwa Zanzibar na taasisi zake ziko chini ya Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 31 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba nitoe maelezo yafuatayo. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba muda wote huo tangu kuanzishwa kwa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwenye majengo yake tumekuwa tukipeperusha bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na bendera nyengine katika majengo ya ofisi zake zote kwa Unguja na Pemba.

Baada ya maelezo hayo, sasa kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kwenye majengo haya ya Baraza la Wawakilishi, bendera zinazopeperushwa kwa kila siku ni tatu na wala sio mbili, ambazo ni bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bendera ya Zanzibar na bendera ya Baraza la Wawakilishi lenyewe.

b) Baraza la Wawakilishi linaangalia taratibu zake, kwa maana hiyo haliwezi kuingilia mamlaka nyengine hasa zilizoko chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi ya Bunge ina mamlaka yake pamoja na utaratibu wake katika kuweka *protocol* yake ikiwemo ile ya kupeperusha bendera kwa kuzingatia maeneo ya kuweka na aina ya bendera.

   Aidha Baraza la Wawakilishi lina taratibu zake na *protocol* zake pamoja na mamlaka yake ndani ya Zanzibar kupitia pia sheria za bendera.

c) Mhe. Mwenyekiti, sio sahihi kusema kuwa Zanzibar na taasisi zake zote ziko chini ya mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani Katiba zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Zanzibar zinatambua mamlaka ya kila upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bendera ya Zanzibar ilipoundwa na kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, Katiba ya Zanzibar ilikuwa ikisema kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, mimi sikuona kuwa kuna kosa kwa bendera ya Zanzibar kama ilivyo bendera ya Polisi ikiwa ni chombo cha Jamhuri ya Muungano, pia kama ilivyo Bunge ikiwa ni chombo cha Jamhuri ya Muungano kwa wakati ule huwa ina kibendera kidogo cha Muungano pale juu.

Kutokana na kwamba tumefanya marekebisho ya Katiba toleo hili la mwaka 2010, Katiba ambayo haimo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyokuwa ile ya zamani.

Kwa hiyo, hatuoni kuwa kupachika bendera ya Jamhuri ya Muungano na kupachika ile bendera ya Zanzibar yenye umbo kimamlaka sawa sawa na Polisi, isipokuwa ni tofauti ni rangi na sawa na bendera ya Bunge ni kuidhalilisha Zanzibar kama ni nchi na mipaka yake. Sasa haioni kuwa hivi sasa umefika wakati Zanzibar kupachika bendera yake ambayo inajitegemea kama Zanzibar ni nchi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ijapokuwa sikumsikia vizuri Mhe. Mjumbe, lakini nitajitahidi nijibu swali lake maana mantiki yenyewe nimeielewa. Lakini naomba tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanapouliza swali la nyongeza waisogelee sana hii *speaker*, ili tuweze kusikia na sisi tuweze kufanya vizuri katika majibu.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, napenda ieleweke kwamba bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatokana na muungano wa nchi mbili, yaani muungano wa Zanzibar na iliyokuwa Tanganyika na tukaunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo, napenda ieleweke kwamba ile bendera ni mali yetu sawa sawa na wenzetu.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Muungano wa Tanzania unatokana na Tanganyika na Zanzibar, lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano haisemi hivyo, isipokuwa inasema Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano, ndipo pale nilipotetea bendera ile yenye kitoto cha muungano pale juu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, napenda tena ieleweke kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatokana na kuungana kwa nchi mbili zilizokuwa huru, yaani Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Watu wa Tanganyika na ikaundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli itakuwa ni jambo la kustaajabisha sana kuwa mpaka leo Mhe. Mwakilishi, haelewi kuwa bendera ile ni haki yetu ni mamlaka yetu kuitumia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine lazima tufike pahala tuelewe kwamba kile ni kitu chetu. Kwa mfano hapa tunadai rasilimali zetu za gesi na mafuta na bendera ile ni yetu pamoja na inapepea umoja wa mataifa kwa niaba pia ya Zanzibar. Kwa hivyo, inapopepea hapa hakuna kosa lolote Mhe. Mwenyekiti, kupepea katika Baraza hili tukufu.

Sasa inapopepea bendera ile, ikapepea bendera ya Baraza la Wawakilishi pamoja na bendera ya Zanzibar ni haki yetu kuitumia, isipokuwa bendera ya Zanzibar ndio mamlaka yetu tu. Kwa maana hiyo, chombo chochote cha muungano hakina haki ya kutumia bendera ile kwa mujibu wa sheria yetu tuliyopitisha hapa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa nimemsikia Mhe. Waziri, akisema kwamba baadhi za taasisi ambazo si za muungano.Kwa hiyo, kutakuwa na maana gani taasisi zile ambazo si za Muungano ama kuweka bendera katika eneo lile au ofisi zile kuwa na picha za viongozi wa Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli zipo taasisi ambazo si za muungano kama Baraza la Wawakilishi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, napenda nirudie tena kwa kuwa bendera ya Jamhuri ya Muungano inatokana pia na Zanzibar yenyewe, yaani mule mulikuwa na bendera yetu kwa maana ile rangi ya bendera inatokana na rangi za bendera ilikuwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Kwa hivyo, tunapoamua kuiweka sio kosa na pia tutakapoamua kuiondoa sikosa, ni haki yetu na lazima tuelewane kwamba hii bendera ya Jamhuri ya Muungano ndio inayojulikana kimataifa. Kwa maana hiyo, ili kulipa sifa na heshima Baraza hili ukiweka bendera ile unaonesha kielelezo safi kwamba Baraza la Wawakilishi linatambulika ulimwengu mzima.

Nam. 4

Biashara ya Madawa ya Kulevya

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Katika maeneo ya Mikunguni, Kundemba, Jang'ombe na Miembeni kumekuwepo na malalamiko ya kuongezeka matatizo ya matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana.

a) Kwa nini serikali isiitishe kura ya siri ya kuwafichua waletaji na wauzaji Zanzibar.

b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejifundisha nini kufuatia kazi inayofanywa na Waziri wa Uchukuzi Dkt. Harisson Mwakyembe kufumua mtandao wa wafanyabiashara ya madawa ya kulevya Tanzania Bara.

c) Watendaji wangapi Zanzibar wamechukuliwa hatua baada ya Mgiriki kukamatwa na unga ndani ya chumba cha kuondokea abiria akiwa tayari kakaguliwa bila ya kuonekana na dawa za kulevya katika begi lake.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 4 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Kwa kawaida katika masuala ya uendeshaji wa serikali, majukumu ya ulinzi na usalama wa nchi yakiwemo ya kupambana na uhalifu wa dawa za kulevya hufanywa na vyombo vya ulinzi na usalama. Vyombo hivi vina mipango na taratibu zake katika masuala ya kuchunguza waletaji na wauzaji wa dawa za kulevya kwa madhumuni ya kudhibiti uhalifu huo hapa Zanzibar.

   Vyombo hivi ndivyo vinavyoelewa ni njia gani sahihi za uchunguzi zinafaa kutumiwa katika mazingira ya nchi yetu. Kwa hivyo, hadi hivi sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijapokea ushauri kutoka katika vyombo hivyo kwamba serikali itumie mpango wa kura ya siri katika kuwafichua wahalifu wa dawa za kulevya.

b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sasa haina taarifa kamili juu ya kazi inayofanywa na Waziri wa Uchukuzi wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania juu ya kufunua mtandao wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Taarifa ambayo serikali imezipata kupitia vyombo vya habari ni juu ya ziara yake ya ghafla ya kuangalia utendaji kazi katika Taasisi yake ya *Airport* Dar-es-Salaam aliyoifanya tarehe 14 Agosti, 2013 na yale aliyoyasema baada ya ziara hiyo kuhusiana na mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Hivyo, serikali bado haijapata jambo jipya la kujifunza kutoka kwake.

c) Katika shauri la Mgiriki huyo zilikuwepo taarifa za awali za kiintelejensia, kwamba raia huyo wa Kigiriki amebeba dawa za kulevya. Kutokana na kuwepo kwa taarifa hizo, Jeshi la Polisi walikuwa wanafuatilia nyendo za mshtakiwa huyo kutaka kuondoka kwake alipoondokea hadi anaingia uwanja wa ndege wa Zanzibar.

Kitendo cha kupita kwenye mashine bila ya kukamatwa kilikuwa kinaeleweka, isipokuwa lengo lilikuwa raia huyo akamatwe akiwa amemaliza taratibu zote za kusafiria, ili aweze kupatikana na kosa la ziada la kusafirisha dawa za kulevya ambalo halipatiwi dhamana.

Kwa hivyo, kama angekamatwa kabla ya kumaliza taratibu ingebidi ashtakiwe kwa kosa moja tu la kupatikana na dawa za kulevya, yaani kosa ambalo angeweza kupewa dhamana na kufanya shughuli nzima ya upelelezi wa kesi hiyo kuwa ngumu. Mhe. Mwenyekiti, hakuna mtendaji ambaye amechukuliwa hatua, kwani hatua ile ilikuwa ni mbinu makusudi za Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inakisaidia vipi Kitengo hichi cha Kupambana na Madawa ya Kulevya ukizingatia kwamba kitengo hichi kinafanyakazi katika mazingira magumu ikiwemo usafiri wanaotumia ni gari ambayo imechakaa sana. Je, serikali inatoa kauli gani.

b) Mhe. Waziri, kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi wanaotusikiliza huko nje. Lini amekitembelea Kikosi Kazi na kusikiliza matatizo yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni mara nyingi sana tokea miaka ya nyuma Kikosi hichi Maalum

cha Kupambana na Dawa za Kulevya ambacho kiko ndani ya Jeshi la Polisi kinafanyakazi kwa ukaribu zaidi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hakika bajeti yake ya kufanyiakazi inatakiwa itoke ndani ya Jeshi la Polisi lenyewe.

Lakini inapotokea dharura kwamba wanahitaji mafuta ya dharura kwa ajili ya kufanya *operation* maalum au kusaidiwa masuala mengine ambayo serikali inayamudu kuwasaidia basi serikali huwa inafanya hivyo. Kwa hiyo, tunafanyakazi kwa karibu sana, isipokuwa bajeti yao ya kufanyiakazi hawa inatokana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Jeshi la Polisi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina bajeti maalum kwa ajili ya kusaidia kikosi hichi, isipokuwa pale inapotokezea dharura basi huwa tunashirikiana nao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ziara kwa mwaka huu mzima sijatembelea kikosi hichi. Lakini katika utaratibu wetu wa Tume ya Dawa za Kulevya, yaani tume yenyewe ambayo inakutana mara kwa mara ina Wajumbe kutoka katika kikosi hiki na ndio wanaotupa taarifa juu ya utendaji kazi wa kikosi hiki. Kwa hivyo, taarifa juu ya utendajikazi wao zipo ndani ya ofisi yangu na serikali inazifahamu vyema. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wahalifu hawa wanaouza madawa ya kulevya ikiwemo bangi huwa wanakamatwa mara kwa mara na kufikishwa Mahakamani. Lakini jambo la kusikitisha hatuwaoni kuchukuliwa hatua za kuadhibiwa kama kufungwa na vyenginevyo.

Je, Mhe. Mwenyekiti, hivi Mhe. Waziri, anahisi huku polisi na Mahakamani kuna tatizo gani mpaka ikawa watu hawa hawachukuliwi hatua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, taratibu za kumshtaki mtu zote zinasimamiwa na chombo kilichohuru ambacho ni chombo cha Mahakama na mara nyingi wahalifu hawa Jeshi la Polisi linafikisha kesi zake na kuzisimamia ndani ya Mahakama na kwa kweli wapo japo ni wachache ambao wamehukumiwa kuhusiana na madawa za kulevya. Vile vile, kesi zake mara nyingi zinachukua mlolongo mrefu wa taratibu za kutafuta ushahidi na kuchelewa kwa kiasi fulani kutolewa maamuzi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ili tuweze kupambana

na madawa ya kulevya, basi lazima tuwe na mashirikiano mazuri kati ya Zanzibar na Tanzania Bara. Jana vyombo vya habari viliripoti rasmi kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeamua kuanzisha sheria ya kuwataja wanaouza madawa ya kulevya hadharani, kwa upande wa Zanzibar tukisema hivyo huambiwa kuna Haki za Binadamu.

a) Je, nini kauli ya Mhe. Waziri, kwamba Zanzibar sisi tuko tayari kuanzisha sheria kuja Barazani ya kuwataja na kuwatambua wanaoingiza na kuuza madawa ya kulevya hadharani.

b) Kama Tanzania imeamua hivyo kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar tukashindwa kufanya hivyo kwa msingi wa Haki za Binadamu, hatuoni kwamba ile dhana ya kimataifa kuwa Zanzibar ni mlango wa madawa ya kulevya itakuwa sahihi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanyakazi kwa ukaribu sana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hususan katika sekta mbali mbali.

Katika suala la madawa ya kulevya, Tume ya Dawa za Kulevya Zanzibar inafanyakazi kwa ukaribu sana na Tume ya Taifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya ya Tanzania.

Kwa kweli suala hili tumelisikia, lakini ni wajibu wetu kwanza kwenda kulitafuta kwa urefu na kujifunza nini faida na hasara yake, ili kama tunaona linafaa nalo tuweze kulitumia ndani ya visiwa vyetu, kwa sababu kwa mujibu wa Sheria yetu ya Kupambana na Dawa za Kulevya hivi sasa wananchi bado wanayo fursa ya kuwataja hawa waletaji na wauzaji wa dawa za kulevya kwa njia ya siri bila ya kuhatarisha usalama wao.

Vile vile, hata katika hali ya kawaida mwananchi yeyote kama anayo taarifa ya mhalifu wa dawa za kulevya basi anaweza akairipoti, kwa ajili ya kuchukuliwa hatua. Kwa hivyo, nasema ni suala la kuweza kujifunza na kulijua kwamba linawezekana kuweza kutendeka hapa Zanzibar au laa.

Kwa maana hiyo, ni mapema mno kujibu swali lake (b) kwa sababu itategemea mazingira ya jibu la (a) kwamba tujifunze tujue faida na hasara yake na kwamba Zanzibar nayo tunaweza kuja na sheria kama hiyo.

Nam. 36

Mkutano Kati ya Rais wa Zanzibar na Vyama vya Upinzani

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jakaya Mrisho Kikwete tangu zamani na hadi sasa amekuwa na utaratibu wa kukutana na vyama vya siasa na hata wapinzani kwa ujumla pale anapohisi kuna jambo aidha la kushauriana au kutoa maelezo, yatakayosaidia kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Je, ni mara ngapi Rais wa Zanzibar amekutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa au hata wale wa Vyama vya Upinzani pekee tangu akae madarakani.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake Nam. 36 kama ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaongozwa Kikatiba chini ya Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa na hivyo kufanya kutokuwa na vyama vya upinzani ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anao utaratibu wa kukutana na Viongozi wa Vyama vya Siasa kila inapohitajika mbali ya kukutana nao kwa miadi maalum. Pia, hufanya mawasiliano ya kimaandishi kila inapolazimika.

Aidha pale sheria inapoelekeza kwamba Mhe. Rais akutane na Viongozi wa Vyama vya Siasa kwa mashauriano,, nalo hilo pia hufanyika. Kwa mfano katika mwezi Machi mwaka huu katika kutekeleza matakwa ya Kikatiba ya kuteua Makamishna wawili wa Tume ya Uchaguzi baada ya kupata mashauriano kutoka Vyama vya Siasa, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi, alikutana na Vyama mbali mbali vya Siasa kwa mashauriano na baadaye kukubaliana na mambo ya msingi katika uteuzi huo.

Mhe. Mwenyekiti, ukiondoa mkutano huo ambao umeelekezwa Kikatiba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, amewahi kukutana na Uongozi wa Chama cha *National League for Democracy* (*NLD*) na uongozi wa Chama cha *Alliance for Tanzania Famers Party* katika nyakati tofauti kuzungumzia mambo muhimu kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, swali linaelekeza ni namna gani Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anakutana na wanasiasa hali inaposababisha kuwa hivyo kama anavyofanya Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Kwa mfano yalipotokea matatizo haya ya Bunge kusema kuwa Zanzibar imeshirikishwa katika Mchakato wa Katiba ya Muungano na vyama vya Siasa vikasema hapana kwenye mikutano ya hadhara, basi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliviita vyama vyote vya siasa wakakutana na wakapitisha maelekezo ambayo kwa maslahi ya taifa.

a) Zaidi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kukutana na vyama vya siasa kwa kushauriana nani ateuliwe kutoka Vyama vya Upinzani. Kisiasa pale matatizo hasa yanapotokea ya kisiasa ni mara ngapi au ni lini alikutana na viongozi hao kwa ajili ya kuweka sawa mambo.

b) Kwa sababu huyu ni Rais tena ni wa nchi haoni kuwa kuna umuhimu mkubwa sana panapotokea machafuko ya kisiasa na sio ya uteuzi ya watu, kwamba ipo haja ya kukutana na viongozi wenzake japo kuwa wanatoka vyama vyengine vya siasa.

c) Swali limeulizwa ni mara ngapi na yeye ametaja mara moja kwa kutuua viongozi na mara nyengine vyama ambavyo ni vya upinzani ambavyo viko nje ya Tanzania. Kwa hivyo, ni mara ngapi amekutana na Viongozi wa Vyama vya Kisiasa wa hapa Zanzibar ndio swali lilivyoulizwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kimsingi maswali yake haya yote naweza kuyajibu kwa pamoja, kwa sababu naona yote yamezunguka hapo hapo. Kwanza kama Mwakilishi naomba afahamu utaratibu ambao Zanzibar tunaendesha nchi yetu na ambao tumekubaliana na nimesema kwenye jawabu langu kwamba Rais wa Zanzibar yeye ana utaratibu wake, hatuwezi kufuata utaratibu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wao Kikatiba wana utaratibu wao, sisi tuna utaratibu wetu kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa mfumo wa serikali wetu. Hilo suala la msingi kwanza naomba Mhe. Salim Abdalla Hamad, ulifahamu na utenganishe.

Kwa hivyo, huwezi kufananisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaratibu wake na wetu anapozungumzia vyama vya siasa, ni viwili tofauti, sisi tuna muundo wetu. Na nimesema mfano hapa sisi hatuna chama rasmi cha upinzani humu ndani ya Baraza. Kwa hivyo, anashauriana na vyama vya siasa kila inapohitajika na nikasema wanafanya miadi, anawaita Kikatiba, kila inapohitajika anafanya hivyo na kutoa mifano miwili au mitatu hiyo ambayo tayari ameshafanya.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeyajumuisha yote kwa pamoja maswali yake kama hivyo. Ahsante.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri, swali la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, wakati anajibu swali mama Mhe. Waziri, ulisema kwamba Mhe. Rais katika mwezi wa Machi alikutana na viongozi wa vyama vya siasa. Je, ni vyama vingapi ambavyo alikutana navyo, ni vyama gani hivyo na bahati nzuri nilikuwepo, lakini si vyama vyote vya siasa vilivyohudhuria. Ni sababu zipi vyama vyengine havikuhudhuria.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, ninakiri ni kweli tarehe ile niliyoitaja Mhe. Rais hakukutana na vyama na yeye Mhe. Hamad Masoud Hamad alikuwepo kama Mwakilishi wa Chama cha CUF na mimi nilikuwepo kama Waziri tu kushughudia lile suala. Ni kweli kwamba hakuviita vyama vyote. Suala la msingi kwamba hivi sasa Tanzania nimejuulishwa kuwa kuna vyama 23 vya kisiasa.

Sasa Mhe. Rais, aliona aviite vile vyama vyenye nguvu hapa kwa Zanzibar kushauriana, angeviita vyama vyote 23 kushauriana jambo ambalo linahusu vyama viwili tu au vitatu tu, kwa kweli ingekuwa haina maana. Walitumia busara kwa kuona kwamba vile vyama vikubwa ambavyo kwa Zanzibar vina wafuasi wengi na vina mvuto mkubwa ashauriane katika suala hili ambalo yeye anahisi wao wanaweza kuwa wadau.Ahsante.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwanza ninashukuru sana Mhe. Waziri anajitahidi kujibu maswali, lakini ninapenda nimuulize kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar ana utaratibu wa kukutana na viongozi wa vyama vya siasa na kubadilishana mawazo na kushauriana au kuchukua mawazo katika maslahi ya nchi yetu.

Na kwa kuwa hivi sasa tuna jambo kubwa mbele yetu ambalo kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inategemea kufanya maadhimisho makubwa ya

miaka 50 ya Mapinduzi ya Serikali ya Zanzibar. Ninapenda kumuuliza Mhe. Waziri, je, Mhe. Rais, amekutana na vyama vya siasa kushauriana na kuwashauri katika kufanya shehere hizo kubwa ili sherehe zetu ziende vizuri na kila mmoja ajione kama ni mwenyewe katika sherehe hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, wazo lake ni zuri kwamba tuna sherehe zetu kubwa za miaka 50 ambapo kila Mzanzibari kwa kweli anastahiki ashiriki kikamilifu kusherehekea ukombozi wetu.

Sasa hili si la Mhe. Rais, hili ni letu sote kama Wawakilishi wa majimbo, sisi ndio wenye wananchi. Leo ninaamini Mhe. Subeit Khamis Faki, naomba radhi tu lakini pengine hatujui au sijui kama ungekuwa Mwakilishi leo hapa kusherehekea miaka 50 katika mazingira tuliyokuwa nayo, ninasema naomba radhi pengine ungeweza kuwa hata Rais.

Sasa ninachosema kwamba haya kuna kamati maalum ya sherehe na mapambo ambayo mwenyekiti wetu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Makamu Mwenyekiti Mhe. Haji Omar Kheir ambaye yeye ndiye Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum, ndiye mwenye watu wote. Kwa hivyo, ninafikiri wazo lako zuri tutakaa naye pamoja tuone vipi wananchi wote wanashirikishwa na kwa kweli tumeshapanga wameshirikishwa na sherehe zimeanza na zinakwenda vizuri sana.

Kwa hivyo, Mhe. Subeit Khamis Faki, niseme wazo lako tumelisikia tutazidi kulichukua kulifanyia kazi kuona kwamba sherehe zetu tunazifanikisha ipasavyo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais naomba niongeze majibu ya nyongeza ambayo yamejibiwa vizuri na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tayari sekreterieti ya sherehe imeshawaandikia vyama vyote kuwataarifu kuhusu suala la sherehe la miaka 50 na kuna utaratibu maalum wa kuwashirikisha ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za miaka 50.

Hata hivyo, tunafanya kila jitihada kutoa matangazo kupitia vyombo mbali mbali vya habari ikiwemo redio na televisheni ili wananchi na viongozi wa vyama vya siasa waelewe ratiba na shughuli zote zinazofanyika. Kwa hivyo, tunachokiomba ni kwa wananchi washiriki katika kila tukio la shamrashamra

za kusherehekea miaka yetu 50 ya mapinduzi.Ninaamini ushiriki wetu ndio utakaofanikisha sherehe zetu hizi. Ahsante sana Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote naomba sana kwa heshima na taadhima uniruhusu japo dakika tatu na kama muda wako utakwenda nitaondosha swali langu huko mbele ili kuzungumza suala ambalo ni muhimu hivi sasa.

Kwanza ninataka kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni kwa kufiliwa na daktari wao *orderly* Bwana Ahmed Issa wa Kituo cha Afya cha Muyuni alichofanya kazi kwa miaka kumi karibu. Vile vile, naomba ma-*orderlies* wawili waliokuwa waja wazito kujifungua kwa usalama usalimini waliokuwepo pale hivi sasa.

Kituo hicho hivi sasa sijui kama hakijafungwa na vile vile sijui kama sijamfanyia haki Mhe. Haji Omar Kheir na hii ninataka niwaambie wananchi wa Jimbo la Tumbatu wamepata Mwakilishi makini anayejali wananchi na kusikiliza kero zao.(*Makofi*).

Hii ndio sifa ya watu wa Tumbatu waungwana, watiifu wafuatiliaji kazi zao. Mhe. Haji Omar Kheir tunakushukuru sana kwa utendaji wako na kulisemea suala hili na kutoa kibali tokea tarehe mosi mwezi wa nane, lakini Wizara ya Afya sijui kwa uzembe au kwa makusudi hawataki kusikia suala hili.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, na kama sikuleta suala hili katika Baraza la Wawakilishi pasingekuwa na daktari pale hadi hii leo, sijui kwa uzembe au kwa makusudi Wizara ya Afya inafanya hivi.

Nam. 45
Kutotekelezwa Agizo la Kuongezewa Muda Daktari wa Hospitali ya Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Hospitali ya Muyuni kwa muda mrefu sana ina tatizo la ukosefu wa Daktari baada ya Dkt. Makame kumaliza muda wake wa utumishi serikalini. Tume ya Utumishi imemuongezea muda wake na miaka miwili kuanzia mwezi wa Agosti, 2013.

(a) Kwanini hakuna utekelezaji wowote wa maamuzi hayo ya Tume ya Utumishi kutoka Wizara ya Afya hadi sasa.

(b) Kwanini hakuna utekelezaji wa maamuzi wakati Tume ya Utumishi kwa kutumia kifungu cha 60(1)(b) cha Sheria ya Utumishi No. 2 ya 2011 imeshaamua kumuongezea Mkataba wa kazi daktari huyo.

(c) Kwa kuwa suala hili hadi Mhe. Rais wa Zanzibar amewahi kuagiza Daktari huyu aongezewe muda na Wizara imeshindwa kutekeleza, nani mwenye maamuzi ya mwisho kati ya Wizara na Rais.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 45 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekitik, kabla sijafanya hivvyo nilikuwa naomba ruhusa kwako niwashukuru Wawakilishi wote kwa michango yao ya rambirambi walionileta, nimeupokea kwa mikono miwili. Ahsante sana.

La pili, naomba nikupongeze wewe kwa sababu naona leo akinamama tupo mbele, sote tunaweza.Kwa hivyo, hongereni.(*Makofi*).

Lakini la tatu, na mimi naomba nichukue nafasi hii pamoja na Kamati ya Muyuni iliyokuja hapa mbele yetu kwa mwenzetu mfanyakazi wa Wizara ya Afya aliyefariki na maziko yatakuwa saa saba. Kwa hivyo, naomba nikimaliza kujibu swali hili uniruhusu na ninaomba kamati tukashirikiane kwenda kumzika mfanyakazi ambaye aliyekuwa anafanya kazi.Baada ya kusema hayo, jawabu ni kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Rais wa Zanzibar kuagiza daktari wa kituo cha Afya Muyuni aajiriwe, taratibu za kumuombea ajira daktari huyo zilifanyika. Wizara ya Afya ilifuata taratibu za kumuombea kupitia Tume ya Utumishi ili kuidhinisha nafasi hiyo.

Kwa vile kulikuwa na maombi mengine ambayo Wizara liliyapeleka kwa ajili ya waajiriwa wapya kwa pamoja tulipata kibali cha ajira hizo ambacho kilitolewa tarehe 07/11/2013. Taratibu za ajira zilifanyika mfanyakazi huyo alijaza mkataba na kuanzia tarehe 1 Disemba 2013 mfanya kazi huyo alikuwa anatakiwa aanze kufanya kazi kituo cha Muyuni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kutokuwa na afya na si ya kweli, uthibitisho huu hapa naomba niisome barua ambayo imeandikwa na Mhe. Omar Haji Kheir.Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti,

"Kwa heshima ninapenda kukuarifu ndugu mtajwa hapo juu ni Afisa Tabibu ambaye amemaliza muda wake wa utumishi na kufika umri wa kustaafu kwa lazima na tayari ameshalipwa stahiki zake. Kutokana na uhaba wa madaktari katika Hospitali ya Muyuni baada ya maagizo ya viongozi wetu tunaomba Ndg. Makame aajiriwe kwa mkataba wa muda wa miaka miwili; kuanzia tarehe 02/08/2013 kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 60(1) (b) kwa sheria ya Utumishi Nam. 2 ya 2011 na *Legal Notice* ya marekebisho yake yaliyosainiwa na Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa taarifa yako Ndugu Makame ni miongoni mwa wastaafu wa Wizara ya Afya waliombewa ajira ya mkataba mapema mwaka huu. Nafunganisha ombi hilo kutoka Katibu Mkuu Wizara ya Afya lenye Na. WA/B90/C Vol. 11/13 ya tarehe 24/3/2013.Aidha ninafunganisha na ombi jipya la *Legal Notice"*.

Huu ni uzembe. Leo ananiambia anaajiriwa tokea tarehe mosi Disemba, barua hii hapa si maandishi yangu yupo tayari kumlipa stahiki zake zote za miezi mitano aliyofanya kazi na kama sikuleta swali Baraza la Wawakilishi pasingekuwa na daktari pale.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kama ifuatavyo.

Maelezo ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Mwenyekiti, tayari yameshatolewa juzi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Naomba kumuhakikishia kwamba suala hili linafanyiwa kazi na kila hatua litachukuliwa ili kila tatizo linalotokezea lirekebishwe katika eneo lile na sio eneo lile tu, lakini Mhe. Mwenyekiti, nia na dhamira ya serikali hii ni kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata matibabu mazuri ili afya zao ziwe nzuri, hayo ndio malengo yetu na ndio malengo ya mapinduzi matukufu ya 1964 watu wetu waishi katika afya njema na tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba tunachukua juhudi kuhakikisha wananchi wetu wanaishi katika hali nzuri, salama na afya njema. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Naomba unaponiambia kuhusu utaratibu, naomba unipe kifungu cha huo utaratibu wenyewe unaotaka kuufuata.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub:Kaajiriwa kishafanya kazi karibu miezi sita au mitano kwa mujibu wa barua hii, ninachouliza haki zake atalipwa au halipwi, tujue kama wananchi tujichangishe kumlipa yule kwa muda aliyejitolea. Nilikuwa ninataka kujua serikali itamlipa haki zake au haimlipi, kama si hivyo wananchi tuchange ili kumuenzi yule daktari tunamuhitaji sisi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo.

Ninapenda nirudie kwamba serikali hii Mheshimiwa nia yake ni kutenda haki na siku zote kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata haki zao. Lakini kwa mujibu wa sheria ziliopo haki zake zote daktari huyo zitalipwa kwa kufuata taratibu.

Mhe. Mwenyekiti, nia yetu kabisa katika serikali ni kuona kila mmoja anatimiziwa haki zake na wananchi na wafanyakazi wanafanya kazi zao kwa furaha na kwa kuwajibika vizuri na haki zao wanapata zote zinazostahiki.
Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nimechanganyikiwa kidogo, sasa sijui nani nimuulize huyu mtu wa mwisho au mwanzo, lakini hata hivyo watalipokea wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais na majibu yake mazuri sana, kwa kuwa hivi sasa wananchi wanaumwa siku hadi siku. Je, Mhe. Waziri ni lini Baraza hili tukufu utalihakikishia kuwa huyo daktari ataruhusika kuweza kufanya kazi wakati huu mara moja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameshalijibu hilo suala. Mwanzo wa awali alilijibu hilo suala. Labda iwe sikufahamu vizuri, lakini naona kama limeshajibiwa.

Mhe. Makame Mshimba Makame: Unaniambia mimi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ndio.

Mhe. Makame Mshimba Makame: Samahani Mhe. Mwenyekiti, amesema kuwa hilo suala litafanyiwa kazi mara moja, lakini mara moja inaweza ika-*take time*, angesema siku maalum, angesema labda baada ya wiki moja au kesho, huyo daktari atarejeshwa. Hilo suala lingekuwa ni sahihi. Ningeomba jibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kama ifuatavyo:-

Kama itakuwa amefuatilia maswali ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, majibu ya Mhe. Naibu Waziri, na majibu ya nyongeza ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais, ni kwamba huyu mtumishi ambaye kama ninamuona pale juu alishaajiriwa kwa mujibu wa *legal notice* ambayo nimeisaini mimi tokea tarehe mosi mwezi wa nane. (*Makofi*).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anachomuombea ni kuweza kulipwa yale maslahi yake ambayo hayajalipwa. Kwa hivyo, upo utaratibu wa kiserikali kwa mtumishi kama huyo akiwa anadai kulipwa malipo ya malimbikizo ya miezi, ndicho Mhe. Waziri wa Nchi alichokisema, lakini huyo daktari tayari yupo na tayari ameshaanza kuwahudumia wananchi. (*Makofi*).

UTARATIBU

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina swali, nina taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tupo katika chombo kikubwa sana. Naomba sana tufuate taratibu na sheria za kuuliza maswali, hatukuja hapa kwenye malumbano Mhe. Mwenyekiti. Tufuate taratibu kwa mujibu wa Kanuni inavyotuelekeza. Ilikuwa nizungumze hayo tu. (*Makofi*).

Nam. 25
Mashine ya Mahudhurio Idara ya Ardhi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Idara ya Ardhi na Upimaji Zanzibar imefunga mashine ya kuhifadhi kumbukumbu kwa watumishi wake wanaoingia na kutoka kazi.

(a) Je, ni kampuni gani iliyopewa zabuni ya kununua na kufunga mashine hiyo na imegharimu kiasi gani.

(b) Kwa nini Idara nyengine na taasisi nyenginezo za Wizara yako hazijafungiwa mashine hizo kama lengo ni kuimarisha uwajibikaji kwa watumishi wa Umma Zanzibar.

(c) Mashine hiyo ina uwezo gani wa kudhibiti vitendo vya utoro kama daftari la mahudhurio limeshindwa kuondoa tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, suala lake Nam. 25 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kufanya utafiti wa gharama na utaalamu wa kufanya kazi hiyo, Idara za Ardhi kwa kushirikiana na Mfadhili wa *SMOLE* walichagua Kampuni iitwayo *GLYN Technology Co Ltd., kutok*a Dar es Salaam kwa gharama ya $1300 kufunga mashine za mlango katika "*Lands House*".

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuna umuhimu mkubwa wa kufunga mashine hizo katika Idara nyengine zote zilizobakia na hali ya fedha itakaporuhusu basi tutafanya hivyo. Mhe. Mwenyekiti, mashine hizo zina umuhimu mkubwa na zina udhibiti wa kuzuia utoro kuliko mfumo huu wa sasa tuliokuwa nao wa daftari, kwani mashine hizo zina uwezo wa kurekodi saa anayoingia mfanyakazi na ile saa anayotoka mfanyakazi, wakati daftari haliwezi kufanya hivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, wafanyakazi wa SMZ wana tofauti gani na wizara nyengine hata akafunga mashine hiyo hapo ya mahudhuria. Swali la pili, mashine hiyo tangu kufungwa imeleta faida gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba kifaa hiki ni kifaa muhimu na kifaa ambacho kinachohitaji gharama, tumeanzia wizara yangu kwa kupitia hii idara ambayo tumeanzia, lakini serikali pindi hali ya fedha itakaporuhusu basi zifungwa katika ofisi nyengine, kwa sababu ni kifaa muhimu, kifaa ambacho kinachodhibiti utoro.Kwa hivyo, hali ya fedha itakaporuhusu basi tutafanya hivyo katika taasisi nyengine.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii nikamuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la ufungaji wa mashine la kuangalia mahudhurio au kurekodi mahudhurio ya wafanyakazi kwa kweli ni suala muhimu. Lakini bado nilikuwa ninataka nijue wizara kabla ya kununua mashine hii iliwahi

kufanya utafiti ni nchi gani ambayo inautumia utaratibu huu wa ku-*register* wafanyakazi wanaoingia na kutoka pale ofisini.

Lakini swali la pili katika utendaji wa shughuli za kila siku katika wizara hii kuna wafanyakazi wengi ambao kazi zao zinakuwa zipo nje ya ofisi. Je, mtu akishaingia kazini na anapotoka hii mashine pia inarekodi pale anapokwenda. Lakini swali la tatu au la (c), ambalo ni la mwisho, je, chombo hichi cha mahudhurio baada ya kuonesha rekodi mfanyakazi kwamba anaingia na kutoka pengine mara nne au tano kwa siku.

Je, kuna hatua gani au kanuni yoyote ambayo inayoongoza utaratibu wa kutoa adhabu kwa mfanyakazi yeyote ambaye atakapokuwa amekiuka zile taratibu ambazo mashine iliyorekodi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu hili swali la nyongeza la Mhe. Hamza Hassan Juma, lenye (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni nia na dhamira ya serikali kuhakikisha kwamba wafanyakazi wake wote wanafanyakazi kwa wakati na wanatoka kazini kwa wakati kwa nia ya kuongeza tija na ufanisi. Na kila hatua itachukuliwa kuhakikisha linafanyika vizuri.

Mimi nichukue fursa hii kuwapongeza wenzetu hawa walioanzisha huu utaratibu wa kuweka vifaa maalum vya kuweza kurekodi wafanyakazi ili waweze kuingia. Ni kweli anavyosema kwamba kunahitaji udhibiti ili hata pale wanapotoka kabla ya wakati wao, hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa.

Ni nia yetu Mhe. Mwenyekiti, kwamba wafanyakazi wafanye wajibu wao vizuri na ndio maana serikali kila wakati sasa inafikiria pia kuwaongeza maslahi ya wafanyakazi kwa msingi wa kuhakikisha kwamba wafanyakazi hao wanawajibika ipasavyo na haki zao wanapata ipasavyo.

Kwa hivyo, ninataka nimuhakikishie Mhe. Hamza Hassan Juma, kwamba hili suala tunalichukua na kwenda kulifanyia kazi ili kufanya tathmini ya wafanyakazi wetu kila mmoja aweze kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizoekwa ili wale ambao watakuwa hawafanyi wajibu wao, hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa na wote tuwajibike kwa maslahi ya nchi yetu na maendeleo yetu.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri, lakini swali langu bado halijajibiwa.

Maana yake nilitaka kujua ni nchi gani ambayo inayotumia mashine hizi, hii jawabu bado sijaipata. Lakini vile vile, je, kuna Kanuni yoyote ambayo inaongoza utoaji wa adhabu kwa wale watakaokiuka ule utaratibu wa kuingia kazini na kutoka, sasa ile pia sikupata maelezo.Lakini maelezo ya Mhe. Waziri ni mazuri, lakini jawabu yangu bado sijaipata.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kama Mhe. Hamza Hassan Juma alivyoeleza.

Mhe. Mwenyekiti, mimi na yeye Mhe. Hamza Hassan Juma, hivi karibuni tulikuwa safarini nchini Marekani na tumeona taasisi mbali mbali kule Marekani zinavyofanya kazi vizuri, kwa maana ya kuweka rekodi za namna hiyo na zipo nchi hata wenzetu Kenya, hata Tanzania baadhi wameanza katika taasisi mbali mbali kuweka utaratibu huu. Kwa hivyo, sio utaratibu mgeni sana, hata hapa Zanzibar zipo ofisini, hivi sasa kwa mfano ghala kuu ya madawa pale Maruhubi wanao utaratibu huu unajulikana pale unapoingia, unapotoka na kila unachokifanya.

Kwa hivyo, kwa ufupi ni wazo zuri na ninataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kadri ya hali halisi itakavyokuwa ya uwezo na matayarisho yakiwa mazuri tuweze kutumia utaratibu huu kwa msingi kwamba utazuia watu kukwepa utaratibu wa kazi.

Na kwa kuwa anazungumzia, je, sheria itaruhusu. Sheria tunatunga wenyewe Mhe. Mwenyekiti hapa, pale tutakapoona wakati umefika wa kufanya sheria hiyo tutafanya hivyo, hata sasa kwa mtu ambaye anayekwepa kazi sheria inaruhusu taratibu za nidhamu zichukuliwe kwa anayekosa kufanya wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Nam. 21

Ukarabati wa Viwanja vya Kabumbu

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Wazanzibari tangu zamani hadi sasa na hapo baadae walipenda, wanaendelea kupenda na watazidi kupenda mchezo wa mpira wa miguu, riadha, *netball* pamoja na *tennis*. Kwa kuwa wachezaji wengi wa Zanzibar hususan wa mpira

wa miguu waliinua vipaji vyao kupitia viwanja vya Mnazi Mmoja na *Mao-Tse-Tung* ambavyo kwa sasa vimo katika hali mbaya sana na wala havifai kwa mchezo huo.

a) Je, ni lini serikali yetu itafanya ukombozi wa wanakabumbu chipukizi kwa kuukarabati Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* pamoja na kuyaondosha maji ya chumvi yanayoingia kwenye uwanja wa Mnazi Mmoja.

b) Ile ahadi ya uwanja wa *Mao-Tse-Tung* kutafuta ufadhili wa ndugu zetu Wachina kujenga imeishia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:-**
Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 21 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wazanzibari wengi wanapenda michezo mbali mbali kama vile mchezo wa mpira wa miguu, riadha, *netball* pamoja na michezo mengine.Mhe.Mwenyekiti, katika kujali na kutambua umuhimu wa kuendeleza michezo hiyo, tayari wizara yangu imekamilisha taratibu za kufanya matengezo ya Uwanja wa *Mao-Tse-Tung*.

Mhe. Mwenyekiti, makubaliano hayo tayari sasa hivi tumeshashirikiana na Serikali ya SMZ pamoja na Serikali ya China kutayarisha michoro na sasa hivi tunasubiri wataalamu kutoka China kwa ajili ya utayarishaji wa michoro na hatua za ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, kukamilika kwa matengenezo hayo kutatoa fursa kwa michezo mbali mbali ambayo itawezesha michezo hiyo kuweza kuchezwa kwenye kiwanja hicho pamoja na kuweka taa ambazo zitasaidia kwa michezo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kiwanja cha Mnazi Mmoja suala hili tayari lipo kwa wamiliki wa eneo hilo ambalo ni Baraza la Manispaa na tayari wanaendelea na hatua zao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Mhe. Mwenyekiti baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri kuhusiana na suala zima la uwanja wa Mao Tse Tung. Katika majibu yake amesema kwamba kwa ushirikiano wa Serikali ya China pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuna mipango ya kufanyia matengenezo uwanja ule.

(a) Je, ni matengenezo gani ambayo yatafanyika katika uwanja ule, ni matengenezo ya nyasi za bandia au nyasi za kawaida.

(b) Kuhusiana na uwanja wa Mnazi Mmoja, ni lini hasa uwanja ule utatengenezwa, hususan tukizingatia kwamba uwanja ule ni ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika hotuba zake mbali mbali kuufanyia matengenezo uwanja ule. Ni lini hasa kwa kushirikiana na hiyo manispaa kuweza kutengeneza uwanja ule kwa faida ya vijana wetu na mpira wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilijibu kwamba kwenye uwanja wa Mao sasa hivi tayari tumeshirikiana na Serikali ya China, na michoro tayari na hivi sasa tunasubiri wataalamu ili kuanza ujenzi wa kiwanja cha mpira cha Mao.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kuwa tumetembelea sisi, kamati ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Serikali ya China, pia na Balozi mdogo wa China aliyepo Zanzibar, kwa kweli uwanja ule utajengwa na kutajengwa paa juu pamoja na mambo yake yote yanayohusiana na mambo ya uwanja.

Mhe. Mwakilishi, ukiwa wewe ni mwanamichezo, basi masuala yote unayajua na sasa hivi wewe ni Mjumbe wa Kombe la Mapinduzi. Masuala yote Mhe. Mwakilishi unayajua na tuko pamoja na wewe. Nataka nikuambie tupo pamoja na uwanja utatengenezwa na vijana wetu wataweza kucheza vizuri mpaka usiku. Kama tulivyoeleza na taa zitatiwa nyingi sana ili vijana wetu waweze kucheza mpira.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nilieleza kuwa kiwanja cha Mnazi Mmoja ni kweli Mhe. Rais aliweka ahadi, lakini kama nilivyokueleza kuwa sisi kwenye wizara yetu, suala lile halipo na lipo kwenye Wizara ya Fedha. Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi kilichopita nilijibu swali hili na Mhe. Waziri wa Fedha akatoa ufafanuzi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, suala hilo lipo na Mhe. Rais ahadi zake huwa anazikamilisha. Kiwanja cha Mnazi Mmoja kitatengenezwa, kwa sababu nilieleza vizuri sana Mhe. Mwakilishi nataka unifahamu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa sijawapongezeni wanawake kwanza leo Baraza letu kuongozwa na wanawake. Mwenyekiti mwanamke, makatibu mezani wanawake. Kwa hivyo, tunawapongezeni, lakini msije kuanzisha mfumo jike.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu naomba liwe kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumezoea kupata ahadi za serikali kila uchao katika kuboresha viwanja vyetu mbali mbali. Nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, ukarabati wa Uwanja wa Amani ndani ya kipindi cha miaka sasa hivi unafanyiwa ukarabati wa mara ya pili. Ukarabati wa mwanzo Mhe. Mwenyekiti, tuliambiwa na aliyekuwa Waziri wa michezo kwamba nyasi za bandia kwa Zanzibar haziwezi zikafaa kwa sababu ya hali ya joto. Leo hata miaka mitano haijamaliza tunarudi pale pale Uwanja wa Amani tunafukua na tunaanza tena kuweka nyasi za bandia.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, suala la Uwanja wa *Mao Tse Tung*, tumekuwa tukipata ahadi nyingi sana za serikali, kila siku Uwanja wa Mao utajengwa na kufanyiwa ukarabati, lakini hakuna kinachofanyika.

Vile vile, Uwanja wa Mnazi Mmoja Mhe. Mwenyekiti, tumepata ahadi kwamba kulikuwa kuna ule mradi wa Wajerumani na mradi ule labda Mhe. Waziri wa Fedha, nilimuona hapa na angekuwepo hapa sasa hivi basi angetusaidia, kwamba kuna ule mradi wa *ZUSP* ambao ulikuwa unatakiwa kuondoa maji machafu katika mitaro mbali mbali likiwemo Jimbo la Kwamtipura na Jang'ombe, lakini vile vile na Uwanja wa Mao. Ahadi hizo zote mpaka leo, hebu tuambieni Mhe. Mwenyekiti, ahadi hizi zitaisha lini ili ionekane kwa vitendo kwamba zinatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri wa michezo kipindi kile alikuwa Mhe. Ali Juma Shamuhuna, alituahidi kwamba angejenga uwanja mwengine ambao ungeweza kupunguza wigo wa Uwanja wa Amani, ambapo uwanja huo vile vile ungeweza kutumia na *indoor games*, na walisema wamo katika mpango wa kutafuta kiwanja mpaka leo ahadi ile hatujui imefikia wapi, labda atuambie Mhe. Waziri, kuwa imefikia wapi. Hizi ahadi za kila siku leo au kesho tutafanya tunataka tuone kwa vitendo. Ule uwanja mwengine ambao ungeweza kusaidiana na Uwanja wa Amani utajengwa lini na utajengwa wapi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, serikali inapoweka ahadi kwa wananchi hujitahidi kama inavyowezekana kukamilisha ahadi zenyewe. Kwa hivyo, serikali inafanya utumishi ambao imetumwa na wananchi, sasa inapofanya hivyo ndio inatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kwanza la Uwanja wa Amani. Uwanja wa Amani unakamilishwa matengenezo makubwa ambayo Wajumbe wenyewe wa Baraza la Wawakilishi hili waliiagiza serikali kufanya hivyo. Katika bajeti iliyopita wizara ikaagiza kwamba itatekeleza maagizo ya wananchi wa Zanzibar kwa kupitia Baraza lako tukufu. Tarehe 19 Disemba, 2013 tukijaaliwa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio mgeni rasmi wa ufunguzi wa matengenezo hayo katika Uwanja wa Amani.

Kwa hivyo, hiyo ni ahadi ambayo serikali imeitekeleza. Sasa ni kweli kwamba serikali huko nyuma ilikuwa na wasi wasi wa *efficiency* ya nyasi bandia. Baada ya kuweka nyasi bandia katika Uwanja wa Gombani Pemba, na tukaona kwamba hazina matatizo, kwa hivyo tukaona ni vizuri sasa tuweke katika Uwanja wa Amani. Kwa hivyo, tulikuwa hatutaki kwa wakati mmoja kuweka nyasi bandia katika viwanja vyetu vikubwa vya serikali halafu tukapata matatizo. Kwa hivyo, tukakiweka kimoja baada ya kugundua kwamba inakwenda vizuri, ndio serikali imekuja kuweka katika kiwanja cha pili.

Kuhusu uwanja wa Mao serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo katika awamu tofauti iliwaahidi wananchi kuwa itatengeneza na serikali hii ya awamu ya saba yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, inahakikisha kwamba itakamilisha ahadi ambayo imewaahidi wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akijibu swali la msingi, ni kwamba tayari serikali imeshakubaliana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, *Memorandum of Understanding* imeshawekwa saini, na tayari tunajua nini kitendo kitakachofanywa katika Uwanja wa Mao. Ile ahadi ya kutengeneza *indoor games* kwa ajili ya michezo mbali mbali nayo imo katika makubaliano hayo ya msingi.

Kwa hivyo, Mhe. Hamza asiwe na wasi wasi ahadi iliyowekwa na Mhe. Ali Juma Shamuhuna, wakati alipokuwa wizara ya michezo, sasa serikali itaitekeleza na tunaahidi kuitekeleza tukijaaliwa, tutajitahidi sana kabla ya mwaka 2015. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Nam. 15

Kugongana kwa Ndege za *Oman Air* na *Ethiopian Airlines*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, mnamo tarehe 1/9/2013 kulitokea ajali ya kugongana ndege za *Oman Air* na *Ethiopian Airlines* katika uwanja wa ndege wa Abeid Aman Karume, Wakati zikiwa zimeshatua. Hali hii inaweza kutia doa suala zima la usalama wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar na kuhatarisha soko la utalii ambalo watalii wengi hutegemea kufika nchini kupitia mlango wa uwanja huo.

(a) Nini kilikuwa chanzo cha ajali ile.

(b) Kuna tatizo la vifaa au uwezo wa wataalamu wetu wa usalam mdogo.

(c) Hadhari gani zimechukuliwa baada ya tukio lile ili lisitokezee tena.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 15 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika tarehe aliyoitaja Mhe. Mwakilishi, tarehe 1/9/2013, ndege ya *Oman Air* yenye namba za usajili A40BB aina ya *Boeing 737* iliigonga ndege ya *Ethiopian Airlines* yenye namba ya usajili *ET-AMG* aina ya *Boeing 767* kwenye bawa lake la kulia yaani (*wing tip*) kutoka upande wa nyuma.

Ndege ya Ethiopia ilikua kwenye maegesho, wakati ile ya Oman ilikuwa inaanza safari ya kuondoka kuelekea kwenye barabara ya kurukia. Majibu.

(a) Mhe. Mwenyekiti, taarifa na Chanzo halisi cha ajali hiyo kitatolewa kwa kupitia chombo cha *TCAA*, kwa sababu chombo hicho ndio muhusika kwa mujibu wa sheria na taratibu husika. Muda huu tayari ripoti husika inaandaliwa na taarifa rasmi itatolewa.

(b) Kwa upande wa vifaa na wataalamu tayari Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeshachukua wafanyakazi 15 wanaotoa huduma ya uegeshaji wa ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Abeid Amani Karume, wamepata mafunzo ya nadharia na vitendo ya uegeshaji wa ndege yaani (*Apron Management*) katika Chuo cha Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania yaani (*CATC)* na kupatiwa vyeti na leseni. Suala la vifaa linaendana na kazi zao.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hadhari iliyochukuliwa. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeagiza ndege zote kubwa ziegeshwe kuelekea usawa wa jengo badala ya kuegeshwa kwa mshazari. Aidha, imewataka wafanyakazi wake wote wajitume kwa juhudi na maarifa, huku utaalamu wao wakiutumia ipasavyo. Hali hii itasaidia ndege kukaa kwa nafasi na kupunguza msongomano. Wakati huo huo serikali inakamilisha ujenzi wa upanuzi wa sehemu ya maegesho yaani (*apron*), utaokamilika mapema mwakani. Kumalizika kwa mradi huu, utapunguza msongomano na kupunguza kwa kiasi kikubwa hadhari kama hizi tulizokuwa tukizizungumza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kutoridhisha ya Mhe. Naibu Waziri, rafiki yangu, swahiba wangu na jirani yangu. Baada ya kutokea ajali hiyo kuna kamati iliundwa inayoitwa *ICAO* ya kuchunguza ajali hiyo, nafikiri mpaka leo uchunguzi wake haujamalizika.

(a) Je, ni lini uchunguzi huo utamalizika.

(b) Kuna taarifa kwa kuwa waongozaji wa alama za ndege pale hawana ujuzi na ni wadhaifu wa utaalamu watendaji hao wa kuongozea ndege. Kwa mujibu wa taarifa za ma- *Captain* zilizopatikana.

(c) Je, unalitolea kauli gani suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimtake sana swahiba wangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, awe msikivu tunapokuwa tukijibu majibu. Ni imani yetu kwamba tunalijibu Baraza na wananchi kwa jumla watasikia.

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yetu tumeeleza kwamba chombo husika ni *TCAA*, chombo hiki ndio chenye mamlaka ya kuunda kamati hii. Kamati hiyo itakapokamilisha ripoti yake. Ripoti tumesema itatolewa na *ICAO* ni chombo cha

kimataifa na *agent* wao hapa wa kusimamia hilo ni chombo cha *TCAA.* Kwa hivyo, unapozungumzia *ICAO* unazungumzia kimataifa na tunapozungumza suala ndani ya nchi *agent* wao ni *TCAA* ndio chombo chenye mamlaka husika. Wanakamilisha utaratibu wa kamati yao waliyoiunda, wakishapata taarifa rasmi basi sisi hatuoni shida wala hatuoni sababu ya kuwanyima, tutawapatia taarifa hizo ili muweze kupata uelewa mpana, tatizo lilikuwa nini, sababu ni zipi na nani mkosa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya msingi tumeeleza kwamba wafanyakazi wetu wanaendelea kupewa mafunzo, kwa sababu kazi hizi huwezi kusema leo, ukahitimu leo na ukawa wewe umemaliza. Kazi hizi kila siku unahitaji kufanya *refresher courses* na ndio maana tukasema tuna wafanyakazi 15 ambao wanafanyakazi za kusaidia ndege katika maegesho, yaani *apron management,* wamemaliza mafunzo yao na kupewa leseni. Ni imani yetu kwamba tutaendelea kuwapeleka wanafunzi hao katika vyuo husika ili waendelee kupata mafunzo kuweza kujikimu na kuhimili kazi ambazo wanazifanya.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa *Oman Air* na *Ethiopian Air* ziligongana na siku hiyo zilipogongana ilibidi zilale na zifanye safari kwa siku ya pili.

Je, kati ya ndege hizo mbili ni ipi iliyoumia na kama kuna ndege moja ambayo ilipata athari ni chombo gani ambacho kiliharibika na Je, gharama ya chombo hicho kilichoharibika kililipwa na Shirika la Ndege iliyogonga au ililipa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar gharama hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba katika siku ile ilipotokezea ajali ndege ya *Ethiopian Airlines* ile ambayo ilikuwa imegongwa ilishindwa kufanya safari zake na wakatuma ndege yao nyengine kuja kuchukua abiria wao.

Mhe. Mwenyekiti, eneo ambalo ndege hiyo ilikuwa imeathirika ni bawa la kulia, walilifungua na siku ya pili walilichukua kwa ajili ya kwenda

kulifanyia matengenezo. Aidha, ndenge ya *Oman Air* iliendelea na safari zake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu ni kwamba baada ya taarifa husika, wao ndio watabaini nani mwenye makosa na nani anapaswa kumlipa mwenzake. Niendelee tu kumsihi Mhe. Subeit Khamis Faki, na Baraza kwa jumla kuwa liendelee kusubiri ripoti ya wataalamu, wao watatuambia nani mkosa na nani anastahili kumlipa mwenzake.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi alisema kwamba taarifa hii ya kitaalamu inafanyiwa kazi na Mamlaka ya *TCAA* Tanzania, ambao sasa hivi wako kwenye mchakato wa kutafuta chanzo cha ajali hiyo. Mhe. Naibu Waziri, ameeleza kwamba wizara yake haitosita kutoa taarifa pale ripoti hiyo itakapokamilika.

Swali langu liko hapa. Je, Mhe. Naibu Waziri, taarifa hiyo itakayotolewa na wizara yako, unakusudia kuitoa kama taarifa katika chombo hiki, au taarifa hii mnakusudia kuitoa kwa utaratibu upi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii hatutoileta hapa rasmi, kama taarifa katika Baraza. Taarifa hii itatolewa kwa umma kupitia vyombo vya habari.

Nam. 16

Usafiri wa Majahazi Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeendelea kuzuia meli zenye uwezo wa kuegesha mchangani kubeba abiria na kusababisha wananchi kusafiri kati ya Pemba na Tanga kwa majahazi na wakati mwengine kuzama.

(a) Je, ni usafiri gani bora na salama kati ya meli aina hiyo na majahazi hadi serikali ikatae usafiri kwa meli hizo.

(b) Vigezo gani vya kitaalamu vimezingatiwa wakati meli hizo zimeundwa na kupasishwa na Taasisi za Kimataifa na kuruhusiwa kuchukua abiria na mizigo.

(c) Maamuzi hayo yanasadia vipi kuimarisha sekta ya usafiri wa baharini kama wawekezaji wa kizalendo wanawekewa mizengwe na vyombo vyao kushindwa kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 16 lenye vifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama sote tunakumbuka kwamba ilitokea ajali ya Meli ya MV. Fatih, tarehe 29 Mei 2009 iliyozama katika Bandari ya Malindi. Aidha, tulipata ajali nyengine ya MV. *Spice Islander* iliyotokea tarehe 9 Septemba 2011 katika maeneo ya mkondo wa Nungwi. Serikali kwa wakati huu imeamua kutoziruhusu meli za aina hiyo yaani "*Land Craft*" kusafirisha abiria. Sababu kubwa ni pamoja na kutokidhi kwa matakwa ya mabadiliko ya Sheria husika. Hasa kutokana na maumbile ya meli hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la majahazi, serikali kwa muda huu haijaruhusu vyombo vya aina hiyo kutoa huduma kwa kuchukua abiria. Bado jahazi halina ruhusa ya kubeba abiria kwani ni kinyume na taratibu za sheria husika.

Kwa hivi sasa serikali inawataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kutosafiria majahazi na vyombo ambavyo si salama, badala yake watumie meli zilizoruhusiwa na kukaguliwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (*ZMA*). Naomba kutoa wito kwa wananchi wetu kufuata taratibu na maelekezo kutoka vyombo na taasisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, jibu (a) na (b) kwa pamoja.

(a) na (b) Mhe. Mwenyekiti, usafiri bora ni ule uliokidhi matakwa na sheria za usafiri baharini pamoja na vigezo vyote vya kitaifa na kimataifa. Yaani usafiri bora ni ule ambao utakuwa umezingatia matakwa ya sheria namba 3 ya mwaka 2009 ya *Zanzibar Maritime Authority*, pamoja na sheria namba 5 ya mwaka 2006, yaani *Zanzibar Maritime Transport Act.*

(c) Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba wazalendo wote wakidhi masharti na taratibu zote kama ilivyo kwa wazalendo wengine wanaofanya biashara hiyo. Sio kweli kwamba kutimiza masharti ni kuwahini wazalendo wafanyabiashara katika nchi yetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri aliyoyatoa kwa muda mfupi hii. Kwa mujibu wa kampuni zilizotengeneza meli za aina ya *land craft* duniani zimepasisha meli hizo kubeba mizigo na abiria.

(a) Je, wataalamu hao na Mhe. Waziri ni yupi mtaalamu zaidi na mwenye akili zaidi.

(b) Majahazi na Meli aina ya *land craft* ni chombo gani kilichokuwa salama kwa kupakia abiria na mizigo, ukizingatia wananchi wetu asilimia 75 ni masikini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, tunachokizungumza hapa meli ambazo hazijakidhi matakwa na masharti ya kiusalama. Hatukuzungumza suala la meli kubeba mzigo na abiria.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kujenga meli mpya Korea, meli ambayo itakuwa na uwezo wa kubeba mizigo pamoja na abiria, msingi mkubwa na kuhakikisha kwamba matakwa na masharti ya kiusalama yamezingatiwa katika meli hiyo.Meli anazozizungumzia Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ni meli ambazo hazikukidhi matakwa na masharti ya kiusalama, kwa sababu meli hizi sio meli ambazo zinakusudiwa kusafiri katika *open sea,* ni meli ambazo zinakusudiwa kusafiri katika maeneo ya ndani, sio meli ambazo zinahimili mawimbi, wala sio meli ambazo zinahimili upepo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kama atakuwa na meli ambazo zitakidhi masharti, serikali haina sababu yoyote ya kuzuia meli hiyo kushindwa kufanya kazi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijatoa ruhusa kwa vyombo vya majahazi kubeba abiria. Chombo chochote cha jahazi kinachobeba abiria, kinafanya kinyume na taratibu na sheria za nchi. Hivyo, naomba

nichukue nafasi hii kuwataka Mamlaka ya Usafiri Baharini kusimamia wajibu wao, kuhakikisha kwamba wananchi wetu hawapandi katika vyombo visivyokuwa na ruhusa ambavyo havikukidhi masharti ya usalama wa usafiri baharini.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya Ukimwi Zanzibar ya 2013

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, aliyetujaalia asubuhi hii tukaweza kufika hapa tukiwa na hali ya afya njema. Pia, tumtakie Mtume wetu Muhammad (*S.A.W*) Rehema na Amani zimshukie juu yake.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo sana kwa mswada huu uliopo mbele yetu; Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya Ukimwi Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu wanaoishi au walioathirika na Virusi vya Ukimwi na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze Mhe. Waziri, na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu wa Kulinda haki za watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni janga ambalo linatukabili takriban dunia nzima. Pia ni suala la muda mrefu na linaendelea kwa kiasi fulani. Kwanza niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma, aliposema kwamba sote ni waathirika. Nakubaliana na yeye, sio kuathirika kwamba sote tuna ukimwi, lakini ni waathirika kutokana na suala hili linalotukabili kwa namna moja au nyengine kila mmoja anakuwa na wasi wasi.

Sio kwa kuwa anakuwa na wasi wasi kwa upande wake yeye peke yake, kwa sababu yeye atakuwa na familia ambayo inamkabili na tuna watoto ambao kila mmoja yuko kwa upande wake. Kwa hivyo, kila mmoja atakuwa na wasi wasi na tukio hili. *Inshaallah* tumuombe Mwenyezi Mungu atujaalie na atupe

mafanikio ya kile ambacho tunakikusudia kukizungumza hapa. Pia, tumuombe Mwenyezi Mungu atusaidie na janga au balaa hili alilotuteremshia.

Mhe. Mwenyekiti, *balaa likija halichagui,* na yote haya yanayotokea kutokana na suala hili, kama Wajumbe wengi waliotangulia kusema kuwa hayasababishwi na mambo ya zinaa tu peke yake. Hii ni balaa, na balaa inavyokuja haichagui ndio maana ikafika pahala ikaathiri mpaka watoto ambao hawana hatia, chanzo hatujui ni nini, lakini yote ni Rehema ya Mwenyezi Mungu hii, linapoingia balaa ndani ya mtaa ikiwa upo au ikiwa hupo basi kwa kiasi fulani kila mmoja inaweza ikamkumba. Kwa hivyo, ni kumuomba Mwenyezi Mungu atusamehe makosa yetu na atuondoshee balaa hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo kujituhumu, hiki ni kitu kibaya sana kwa mwanadamu, kweli tunao watu wanaoathirika na ukimwi, wanaoishi na hivyo virusi lakini watu hawa hujihisi wao badala ya kuona matokeo yale yamewafikia hujiona kama ni watu waliofikiwa na majanga gani. Kitu ambacho kuna maradhi mengi mbali mbali ambayo yanakuwa mtu akiyapata hategemei kupona, lakini wapo na wanaishi ndani ya familia zao.

Lakini leo mtu akisikia kuwa amegundulikana na suala hili na yeye mwenyewe hufanya tuhuma, ina maana anapokwenda popote, anavyofanya vyovyote, akitizamwa na mtu hata kama hajafanyiwa pengine vitendo vya kunyanyapaliwa, lakini basi yeye mwenyewe huwa anajituhumu kwamba yule ananitazama miye au ananisema miye. Ningeomba sana wale ambao Mwenyezi Mungu amewajaalia kwa njia moja au kwa namna nyengine, kufikwa na majanga haya basi kwanza waache tabia za kujituhumu wao wenyewe ili badala ya kupata ushauri nasaha waweze kuishi maisha mazuri na ya matumaini.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu na kifungu cha 8 kinachosema taarifa na elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi katika sehemu za kazi. Kama tunavyosema kuwa suala la ukimwi ni suala la muda mrefu, na ni suala linaloendelea siku hadi siku. Kuhusiana na masuala ya elimu nadhani elimu imeshatolewa nyingi sana, lakini bado hatutajua hatima ya suala hili. Lakini na hao wafanyakazi wanaotakiwa kupewa elimu ambao kuwa wameandikwa hapa

Kifungu cha 8(1) (a) "wafanyakazi wote walio kwenye Utumishi wa Umma, na

(b) Wafanyakazi wa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na vikundi vya jamii."

Humu mote nahakikisha kuwa elimu zimeshapatikana. Lakini elimu zilizokuwa zikitolewa zilikuwa haziwafikii jamii kwa ujumla, hawa wanaoishi vijijini. Elimu hizi zilikuwa zikitolewa, ilifika pahali mpaka zikawekwa ofisi zile za *ActionAid* kila shehia, lakini mafanikio hayakupatikana.

Suala hili kila linapotolewa tathmini unaambiwa ukimwi bado haujapungua hata kidogo. Tukisema tunaambiwa kwa kuwa watu wanahamasishwa wanakwenda kupimwa ndio maana ikabidi wanagundulikana na hivi virusi, tofauti na huko nyuma tunakotokea. Mimi nakubaliana nalo hilo, lakini pia nasema na elimu iliyokuwa ikitolewa haiwafiki walengwa.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi au watu wengi wanaoishi mijini ni wepesi sana kupata taarifa hizi kwa njia zinazotumika. Kwa sababu taarifa zinazotumika pengine ni za redio, televisheni na katika warsha mbali mbali. Lakini zile warsha zilizokuwa zikifanywa ilikuwa ni wale wanaokwenda kule tu kufanyiwa semina zile au makongamano yale wanaporudi wanabakia majumbani mwanzo, hawatoi hiyo elimu waliyoipata kule. Ukiangalia watu tuliokuwepo vijijini sio wengi ambao wana muda hata wa kusikiliza hiyo redio.

Sasa basi, katika utoaji wa elimu ambao kuwa mmeukusudia hapa sasa hivi, ningemuomba Mhe. Waziri, aandae katika kamati zao Shehia ambazo wanategemea kuziunda waoneshe filamu zenye micheto mbali mbali kama zile zilizokuwa zikiitwa sinema bubu zilizokuwa zikipita ndani ya magari. Nahakikisha tutakapofanya hivi elimu itapatikana hasa maeneo ya kwetu sisi vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mmoja kuna Ustadh mmoja ni muuzaji wa dawa, anatoka Bara anakuja na dawa zake na yeye ni mfanyabiashara, anakuja pale kwa kutoa mawaidha na anabakia msikitini. Lakini anapokuja pale anapotangaza mawaidha kwamba yatakuwa muda fulani, watu walikuwa hawaendi. Lakini ikifika usiku saa 2 alikuwa tayari akiweka *TV* yake akionesha *CD* za visa vya Mitume basi watu walikuwa wanakuja kwa wingi, wanakaa mpaka saa 6 za usiku, kike na kiume. Kilichowavutia pale ni nini.

Ni zile *CD* ambazo zilizokuwa zikioneshwa. Sote ni Waislamu, mawaidha nayo ilikuwa ni haki yao kwenda kusikiliza lakini pale kwenye *TV* walikuwa wakifuata ile *CD* na ile michezo iliyokuwa na visa vinavyooneshwa. Na nyie nawaomba mfanye hivyo, muunde Kamati zenu kama ni za Wilaya, muandae vipindi vyenu vizuri ambavyo mtu akiviona vitaweza kumuelimisha na kuweza kupata angalau *idea* fulani, kwa upande wa vijijini hilo litatusaidia.
Suala la pili kifungu cha 10 taarifa ya elimu na ya virusi vya ukimwi na ukimwi katika jamii.

Kifungu cha 10(1) "Tume na wadau wengine ikijumuisha vikundi vya kijamii na taasisi za dini, utamaduni na viongozi wa kijamii, itaelimisha jamii juu ya hatari ya vitendo vya kitamaduni ambavyo ..."

Mhe. Mwenyekiti, imekusudiwa hapa ikijumuishwa hivi vikundi vya kijamii ikiwemo taasisi za kidini kuhamasisha watu au kutoa mihadhara na kuzungumzia suala zima la tatizo hili. Lakini viongozi wa kidini watakapokwenda wao wakaweka mihadhara yao katika kujumuisha hili, wao hawatozungumzia kuwaambia waislamu kuwa hili ni tatizo linalotukabili kwa hiyo mtu anayetaka kufanya kitendo hiki basi atumie kondom. Hili kwa taasisi za dini naona halitokuwa rahisi kulizungumza hilo. Kwa sababu katika kifungu cha 9(a) kinasema hivi,

Kifungu cha 9(a) "kuongeza uelewa wa Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kama ni suala la haki za binaadamu"

Limechukuliwa kama ni suala la haki za binaadamu. Pengine viongozi wa dini watakapokuja kuweka mihadhara wakazungumzia hali halisi na wakakataza yale maamrisho ambayo Mwenyezi Mungu kayakataza. Mhe. Waziri, je, nikuulize na huku umeshasema kuwa Ukimwi ni suala la haki za binaadamu. Watu hawa hawaji kwenda kuchukuliwa, ikaja ikawa watu hawa wameshawanyanyapaa wanaoishi na virusi vya Ukimwi.

Naomba unieleze kifungu hichi na uwaeleze watu wasikie, kuwashirikisha watu wa dini katika hili, mtu wa dini hatokuja hata siku moja akatoa maelezo yake halafu akasema kwamba watu wavae kondom, kwa kuwa dini haijatuelekeza kwamba tufanye hivyo. Dini imetukataza kufanya tendo ambalo ni chafu. Sasa atakapokwenda kukataza yeye na wewe sheria yako imeshasema kwamba masuala ya Ukimwi ni haki ya binaadamu. Wale Mashekhe hawajikuchukuliwa pale.

Nakuomba Mhe. Waziri, unipe maelezo katika suala hilo na kifungu hicho kilivyokusudiwa.Nikiendelea na mchango wangu katika kifungu cha 15 kimezungumzia hapa nataka unipe ufafanuzi juu ya kifungu hicho.

Kifungu cha 15(1) "Kituo au mtu amepima Virusi vya UKIMWI atalazimika wakati wote kutoa ushauri kwa watu kabla na baada ya kumpima Virusi vya UKIMWI. Kwa upande wa mtoto au mtu mwenye ulemavu...."

Miongoni mwa kifungu hichi na kifungu cha 18 kupima virusi vya ukimwi, ambacho kifungu cha 8(1) kinaeleza"

Kifungu cha 18(1) "Mtu haruhusiwi kumpima mtu mwengine Virusi vya UKIMWI mpaka mtu huyo awe ameruhusiwa kufanya hivyo na Waziri anayehusika na Afya"

Sijui ulichokusudia hapa ni kuwa haruhusiwi kupima mtu kumpima mtu mwenye virusi vya ukimwi au haruhusiwi mtu kufanya nini. Naomba kifungu hichi na hichi chengine naomba unipe maelezo kidogo naona sijakifahamu kidogo.

Nikiendelea mbele Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nipewe maelezo hapa kifungu cha 23 mpaka 24 Sehemu ya Sita kinasema hivi:

Kifungu cha 23(3) "Mtu ambaye atakuwa amebaguliwa kutokana na kuishi na kudhaniwa kuwa ana Virusi vya UKIMWI, anaweza kufungua kesi ya madai dhidi ya mtu anayembagua na kudai fidia"

Kifungu cha 24(1) "Kila mtu atastahiki faragha ya kufichiwa siri kuhisiana na hali yake ya UKIMWI"

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kifungu hichi tumewafanya kama hawa waathirika wao hawawezi kufanya kosa lolote wao pengine dhidi ya watu wengine waliokuwa hawajaathirika. Mheshimiwa kuna watu hao wanaoishi na virusi vya ukimwi wengine wanakuwa hawana tabia nzuri. Pengine ataona yeye tayari ameathirika, lakini badala ya kuona yeye keshaathirika hatakiwi kueneza kwa wengine. Sasa hawa tusiwafanye kuwa wao walioathirika kwamba hawana kosa hata moja ambalo kuwa wanaweza kulifanya. Na wao kuwa wanaweza wakawa na makosa wanaweza kuyafanya.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mtu kama huyo akija akibainika kuwa yeye tayari anajulikana kuwa ameathirika, lakini katika mbio zake akataka kueneza na watu wengine na yeye atafanywa nini? Tusiwafanye wao kama ni malaika wao, hawa na wao ni watu na ni binaadamu na kila mmoja ana tabia zake. Wasionekane wale tu ambao akimtizama ataonekana kamnyanyapaa, na wao pia wanakuwa wengine wana tabia si nzuri.

Kwa sababu yeye tayari keshaathirika na afuate taratibu za kisheria zinazomuelekeza, kama yeye majanga yale yameshampata basi kuna wengine wapo kule kama yeye wanaweza wakaoana, sio ajifiche mitaani halafu akawa anapita anausambaza zaidi ya wale. Je na yeye akibainika afanywe nini. Mhe. Waziri, tunaomba hapa atueleze.

Mhe. Mwenyekiti, na kifungu hiki pia naomba nipatiwe ufafanuzi.

Kifungu cha 36(2) "Mtu yeyote anayetaka kufanya utafiti kuhusu UKIMWI utakaomuhusisha binaadamu atalazimika kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Bodi au Taasisi nyengine yoyote iliyoanzishwa na Wizara inayohusika na masuala ya Afya"

Hapa nilikuwa nataka nijue Mhe. Waziri, huyu anayetaka kufanya utafiti pengine amegundua dawa fulani au kufanya utafiti ya kuwa wenye *dispensary* hawaruhusiwi kuchunguza masuala haya ya Ukimwi. Naomba na hili unieleze ni utafiti unaohusiana na nini ambao unatakiwa upatiwe kibali cha maandishi kutoka kwa Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nije kwenye madhumuni, kwenye ukurasa wa mwisho, kinaitaka serikali kwa kushauri na Tume, kuandaa na kutekeleza mikakati, sera na mipango ya kuimarisha na kulinda afya za makundi hatarishi na watu wanaoishi katika hatari zaidi ya kuambukizwa.

Huku chini umewataja kuna umasikini, maisha yao, utumiaji wa dawa za kulevya, uasharati na mambo mengine kadhalika. Mhe. Waziri, hili nakubaliana na wewe, makundi haya yapo kwa asilimia kubwa. Kwanza tukienda kwenye umasikini ni makundi yaliyokithiri na yapo vijijini ambapo kama nilivyokwambia mwanzo hata hizo elimu haziwafikii. Makundi haya ni mengi ambayo pengine yamo katika hatari zaidi ya kuambukizwa hasa sisi wanawake tunaokaa vijijini.

Kuna watu hatuna elimu, lakini kuna watu ambao pengine tuna waume zetu wanaokwenda Mabara huko wakakaa miaka miwili na mitatu tukija hatujui la kufanya isipokuwa ni mapenzi kuendelea mbele. Naomba elimu hii kama nilivyokueleza mwanzo nilivyozungumza basi utusaidie sana Mhe.Waziri, siye tunaoishi vijijini.

Lakini pia na kuhusu hawa wanaotumia dawa za kulevya nao pia ni wengi. Na hawa wa uasharati ni wengi, watu kama wanavyosema wenyewe wamekuwa kama ni kuku wanaochumia midomo yao, wanahitaji elimu ya kutosha ili tuweze kutokana na janga hili ambalo kuwa Mwenyezi Mungu ametujaalia nalo. Kwa hayo, machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono Sheria hii lakini pia na kuweza kunipa ufafanuzi juu ya masuala yangu niliyokuuliza uje unieleze, na unambie vipi utatusaidia watu tunaoishi vijijini. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Abdalla Moh'd Ali, nilikuwa nakuomba kuna Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa anatakiwa kuhudhuria kwenye kikao saa 5. Kwa hivyo, nilikuwa naomba uniruhusu nimuachie yeye achangie na baadaye utafuata wewe.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia mawili matatu na baadaye niweze kuelekea juu kwenye Kamati ya Uongozi ili tuweze kuendelea na utaratibu wetu wa utendaji kama ambavyo tumejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii vile vile, kumshukuru, swahibu yangu, rafiki yangu Mhe. Abdalla Moh'd kwa kukubali lile ombi ambalo amempatia. Mimi nianze na hili suala la la Ukimwi. Mimi leo sitaki kutembea katika vifungu hasa, naomba kwenda kwa ujumla wake nitafuta baadhi ya vifungu tu kidogo kidogo lakini naomba kwenda kwenye ujumla.

Maradhi ya ukimwi yalianza kuonekana katika nchi yetu ndani ya miaka ya 1980. Mzee wetu Rais Mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi, alikuwa ana usemi wake wa ishtizai anasema kwamba "*Maradhi haya yameingia pabaya*" au "*Asali imeingia sumu*" na kule kwetu Pemba kuna neno linasemwa kwamba "*haya maradhi yameingia kwenye panda na panda yenyewe ina pango*" .

Mhe. Mwenyekiti, suala la Ukimwi ni suala zito na lina athari katika jamii yetu. Linaharibu mustakbali mzima wa taifa la kesho. Mimi nilipata bahati ya kuhudhuria katika mikutano miwili ya Ukimwi ya hivi karibuni. Mkutano wa kwanza ulikuwa wa *ZAPHA+* ambao ulifanyika kwenye mtaa wa marehemu Mzee Saidi Washoto, Amani, ambapo mkutano ule ulihudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Lakini pia, niliweza kuhudhuria katika mkutano uliofanyika Paje wa Sherehe za Ukimwi duniani. Katika kile kikao cha pale kwa Mzee Saidi Washoto tulipata takwimu ya watoto ambao wameathirika na wana virusi vya ukimwi, watoto wale ile idadi kamili sikuwa nayo hivi sasa hapa, lakini walikuwa wanatembea nao ni zaidi ya 50 au ni zaidi 500. Tayari ni waathirika wa maradhi ya ukimwi.

Vile vile, takwimu ambazo zilikuwa zimetolewa shamba Paje, tumetoka kwenye asilimia 0.4 mapaka sasa tunaelekea kwenye asilimia 1. Hii inaashiria kwamba haya maradhi yanakuja kwa kasi kubwa mno. Nini kifanyike.

Nimeangalia katika Mswada wetu ambao tumepewa Waheshimiwa Wajumbe, nimekuta tumejipanga zaidi katika suala zima la kukabiliana na hawa watu ambao tayari wamekwishaathirika na virusi vya ukimwi au na ukimwi

wenyewe. Sikuona mikakati ya kuangalia ni jinsi gani tunafanya *prevention* kwa watu ambao hawana maradhi haya ya ukimwi ili wao wasije wakaathirika na maradhi haya. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atusaidie na hili alipe umuhimu wa aina yake. Suala la kufanya tahadhari kabla ya athari haijatutokezea na kutukumba kwa namna ambavyo kasi hii ya maambukizi ya ukimwi imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukimwi katika nchi yetu ya Zanzibar, mimi kwa utafiti wangu ambao nimeufanya, nimeona unasababishwa zaidi ya janga la umasikini, rushwa na ajira. Kutokana na umasikini watu wetu wanathubutu kudhalilika na kupelekea kuweza kufanya mambo ambayo hayakidhi na wala hayastahiki. Kwa mfano ndugu zetu akina mama hawa ambao nyakati za usiku katika maeneo fulani fulani huwa wanakwenda na kufanya biashara zao za kuuza miili yao. Wale wanaokwenda kufanya biashara zile huwa hawawajui kama mfano ni waathirika au laa.

Kutokana na shida yao ya umasikini imesababisha kuweza kufanya mambo ambayo yanaweza kusababisha maisha yao kwa ujumla wao. Ningependa tutengeneze mikakati imara ya kuhakikisha kwamba watu wetu hawa tunawatengenezea mustakbali mzuri ili waweze kuondokana na biashara hii ya kubahatisha ili waweze kuishi katika maisha ya salama ndani ya nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni rushwa. Kusema kweli rushwa ni jambo ambalo linasababisha maradhi haya ya ukimwi yaweze kuendelea kwa kasi kubwa. Tatizo la rushwa sote tunalielewa, naomba vyombo vinavyohusika kuchukua juhudi za lazima kuhakikisha kwamba hii rushwa nayo angalau inachukuliwa hatua na kuona watu wetu wananusurika na maradhi haya ya ukimwi kwa asilimia ya kasi ambayo inaendelea siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, ambalo nilikuwa nataka kulichangia ni suala zima la ubakaji. Zanzibar kwa sasa na Tanzania kwa ujumla tumekuwa tuna wimbi kubwa la ubakaji kwa sasa. Sifa ambayo katika Visiwa vyetu na Tanzania yetu hapo mwanzoni tulikuwa hatuna. Sijui ni kitu gani kimepelekea kwa sasa kadhia hii imeongezeka kwa kasi kubwa. Ningeliomba taasisi zinazohusika hususan Mahakama pale zinapopelekwa kesi zinazohusiana na masuala ya ubakaji na udhalilishaji, sheria zitumike na Mahakama ziondokane na utaratibu huu ulioko sasa ambako hata wananchi wa kawaida wanapoteza imani na Mahakama kutokana na rushwa kushamiri sana katika vyombo vyetu vya kutunga sheria.

Mhe. Mwenyekiti, kesi za ubakaji zimekuwa nyingi. Juzi nilikuwa naangalia taarifa kulikuwa kuna mwanasheria mmoja alikuwa anahojiwa na kituo cha *ITV* pale Dar-es-Salaam, yeye ni mwanasheria na ni mtu wa Uhamiaji.

Amesema katika eneo la Ilala tu peke yake kuna kesi za ubakaji 75. Watu hawa wamebakwa katika kipindi kifupi tu, hii ni hatari. Lakini bila ya kusahau ni juzi tu ndani ya jimbo langu mwenyewe la Kikwajuni kuna wanafunzi wanaokwenda kusoma maeneo ya Miembeni, wakati wanarejea kuja makwao maeneo ya Migombani walikuja akapakiwa lifti baadhi yao, wakapakiwa na gari wakapelekwa makwao, mmoja akawa ameshindwa kupanda ile gari kwa sababu ilikuwa imejaa akawa anatembea peke yake.

Huyu mtoto kwa taarifa niliyoletewa na mmoja kati ya wazee katika maeneo yale ni kwamba yeye ilikuja gari ikampakia ya vijana, vijana hao tayari tunawafuatilia na tutakapopata taarifa zinazohusiana na taratibu za kuchukua kisheria tutakwenda kunakohusika tuone hatua za kisheria zinachukuliwa ili tutoe adhabu kwa hawa ambao wanahusika.

Kijana yule alipakiwa ndani ya gari na akapelekwa njia ya Buyu akaenda akabakwa, akarejeshwa saa 8 za usiku. Suala hili tunalifuatilia halafu baadaye vyombo vya habari na vyombo vya sheria vinavyohusika vitaendelea na taratibu zake. Sasa hatuna yakini miongoni mwa wale wabakaji ni nani na nani ambaye anahusika na masuala ya maradhi haya ya ukimwi. Ina maana mpaka maisha yake yule mtoto ambaye ni mdogo sana yuko chini ya miaka 24 na yeye vile vile, huenda ikawa anaweza akawa ameathirika na matatizo kama haya.

Hatari iliyokuwa ipo ndani ya jimbo langu hili hili la Kikwajuni katika kituo cha Madema kuna kesi ambazo ziliwahi kupelekwa pale za ubakaji lakini matokeo yake, hili tulizungumziwa juzi katika semina. Yule mtoto amepelekwa pale kwa kesi ya ubakaji, lakini hapo hapo na yeye akabakwa tena hapo hapo kituoni kwa sababu amekwenda katika sakata la ubakaji. Hili lilikuwa ni jambo moja zito sana. Yule mtu ambaye amekuja kutuletea ile kesi pale tulimwambia kwamba hili tutalifanyia kazi vile vile.

Sasa huu ndio uhalisia wa hali yetu inavyokwenda ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Ningeliomba sana chombo hiki cha ulinzi na usalama katika jeshi la Polisi kwa kusaidiana na mahkama lakini zaidi na wananchi sote kwa ujumla wetu, hebu hili suala la ubakaji tulivalie njuga na tuone kwamba tunaishindikiza serikali na tuone sheria inachukua mkondo wake na udhalilishaji unakwisha mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nilikuwa naomba kuchangia ni kuiomba Wizara inayohusika kuharakisha upatikanaji wa kifaa cha *DNA* ili tuone kwamba wale watu ambao wanahusika na kadhia hizi wanadhibitiwa kwa kupatikana ushahidi. Kwa vyombo hivi vinaweza kusaidia kupatikana na

kutiwa hatiani kwa mtu ambae ana tatizo ambalo limesababisha matatizo ya kuweza kupatikana na kosa kama hili.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti ningeliomba zile kesi ambazo ziko katika mahkama zetu ziendeshwe kwa mujibu wa taratibu za kisheria, na pale ambapo wananchi wetu wanyonge wana haki ya kupewa katika mambo ambayo yanahusiana na mahkama basi wapewe hata kama hawana uwezo wa kutoa kile kima cha fedha ambacho anatakiwa kulipia ili waweze kupata haki yao kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima naunga mkono hoja hii endapo maombo yangu na maoni yangu yatafafanuliwa na yataelekezwa kwa kina kwa mustakbali wa kuleta maendeleo ndani ya nchi yetu.

Baada ya maelekezo hayo naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru kunipa fursa ya kusema machache na mafupi sana katika sheria hii. Kwanza ninafikiria kwa vile wewe leo ndio mwenye rungu hapo ulikuwa huna sababu ya kuniomba, ninafikiri ungetumia wajibu wako tu wa kumwita Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, akaanza kuchangia baadae ningelifuatia mimi bila ya tatizo lolote. Lakini ninakushukuru kwamba umenipa heshima yangu na naomba uiendeleze.

Mhe. Mwenyekiti, tupo katika kuchangia sheria ambayo kidogo kwa maoni yangu imegusa eneo ambalo mimi kama ni wajibu wangu napaswa kidogo kutoa *reservations* zangu. Kwa ujumla sheria sio mbaya lakini tu hayo maeneo ambayo yameyafika itabidi na mimi nipato maelekezo na niyazungumze kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, ninafikiri una kumbukumbu kwamba ni mwaka huu tulipitisha sheria ya mtoto, sheria ambayo ninafikiri ilitunyima fursa wazee ya kupata msaada kutoka kwa vijana wetu ambao wana uwezo labda wa kutusaidia kwa njia moja kupata vijio. Lakini pia ninasikia kuna ndumu ndumu kwamba kunakuja sheria ya kuhalalisha au kuridhia Tanzania ya wanaume kupata fursa ya kuoana. Jana katika semina tulipata fununu kwamba na sheria hiyo ilitakiwa na Tanzania nayo iiridhie.

Lakini pia, nina wasiwasi na sheria ya wanawake ya kuwa tugawane mirathi sawa kwa sawa huenda ikaja katika Baraza lako Tukufu. Mhe. Mwenyekiti, sheria hizi zote kwa uoni wangu kidogo zinatofautiana na imani zetu au imani yangu.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria yetu kubwa inayotuongoza inatuambia kwamba sisi hatutakiwi kuipeleka mikono yetu katika maangamizi, tumeambiwa kwamba *walaa tulku aidiakum illa stahluka*. Sasa sheria ya ukimwi tuliyonayo hapa na nikiangalia zile sababu ambazo zinapelekea mtu kupata matizo haya kidogo ninahisi sheria inataka kuwalinda watu ambapo sheria yetu mama hivyo. Kwa mwongozo huo ningemuomba Mhe. Waziri, au serikali kwa ujumla wakati wa kuleta sheria ikazingatia hay.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa imekuwa ni hivyo na naomba nikumbushe tu kwamba sisi tumeambiwa kwamba kuna kundi la watu halitoridhika mpaka watapohisi au watakapojua kwamba tumewafuata zile mila zao na desturi zao. Ninafikiri sasa Mhe. Mwenyekiti, tunaelekea huko kwamba mila zao tunatakiwa sasa tuzifuate na ndio maana kila sheria zinazokuja za Umoja wa Mataifa tunatakiwa tuziridhie ili tuwaridhie na wao, sheria tukufu ipo inayotuelekeza, sheria mama ipo naomba tuizingatie kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii kuna kipengele kinachosema kwamba hivi sasa tunatakiwa tueneze elimu ya mambo ya ukimwi katika sehemu za ibada. Mimi ninaomba nikumbushe tu kwamba sheria yetu tukufu tayari imeshalisema jambo hili kwamba sisi tunatakiwa tukumbushane mema na tukatazane mabaya. Sasa mimi wasiwasi wangu kwamba sheria hii kuifanya kwamba lazima tupeleke elimu katika sehemu za ibada, jirani yangu Mhe. BikameYussuf Hamad, na yeye kakiona kipengele hicho kwamba itafika wakati itakuwa sasa tueleze mambo ambayo ni kinyume na imani zetu.

Ninafikiri mimi ningemshauri Waziri hizi sehemu za ibada basi zikaondoka kwa vile tayari zipo, wale watu ambao wanajua wajibu wao wa kila siku, masheikh wetu na maamuma wetu wanafahamu linalotokea katika mtaa, kama wanaona litakuwa na umuhimu leo waje wakae katika viriri, wazungumze suala la ukimwi, basi watazungumza. Sasa mimi wasiwasi wangu na naomba Waziri anihakikishie hivyo kuwa sheria hii hatutofika wakati tukawa hotuba zetu za Ijumaa zinatungwa katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na tukalazimika leo lazima tuzungumze mambo ya ukimwi nina wasiwasi.

Sasa kwa mnasaba huo ningependa Mhe. Waziri, hii sehemu inayoitwa sehemu za ibada iondoshwe, ninafikiri masheikh wetu wanajua wajibu wao na wanajua linalotokea katika mazingira na wanachokizungumza kitahusiana na ile jamii. Lakini kukiweka hivi mimi sioni kwamba kitaleta mnasaba mzuri hasa ukizingatia mwisho wa kuuzungumza ukimwi ni kujilinda. Kujilinda kwake Mhe. Mwenyekiti, ni kutumia vyombo ambavyo vitahakikisha kwamba wewe hupati maradhi haya.

Lakini kufanya hivyo ukiieleza jamii ni kwenda kinyume kabisa na dini yetu na imani yetu. Na nina imani kwamba wengi tuliomo humu tuna imani hiyo hiyo hatuna imani nyengine. Sasa ningeomba sehemu hii ili isije ikazua mizozo ambayo tayari imo katika sehemu zetu za ibada. Basi sehemu hii akaifuta na akaendeleza tu sehemu nyengine kama ni shule, na wengine jana wameshapendekeza katika sheria zetu huko kwamba tunapotunga sheria tuangalie jinsia pengine hata mashule, yatakuwa yapo tofauti kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni; wanawake kwao na wanaume kwao. Sijui kama hilo litapita, lakini katika kuzingatia jinsia mmoja jana alipendekeza suala hilo.

Sasa ninahisi na sheria hii ingeliangalia hilo kwamba ili kuondoa hiyo mizozo basi hizi sehemu za ibada tuziachilie kwa kuhofia kwamba kama unampa fursa hii basi inawezekana na mwengine akaja akaomba fursa kwamba sasa na yeye atataka kuzungumza mambo yake mengine. Sasa kuepusha hayo naomba Mhe. Waziri, hii sehemu ya ibada akaiacha, wajibu wa dini yetu ni kukumbushana mabaya na kuelekezana mema, kama hayo yanafikia katika sehemu ya kuwa masheikh waeleze watayaeleza hatuna haja ya kuyaweka katika sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii vile vile inatuelezea kwamba mambo haya yote yanatakiwa yawe siri, ukishamgundua ambae atakuwa na matatizo haya basi unatakiwa wewe ufumbe mdomo, macho na mengineyo, usinyooshe kidole kwamba yule hivi hivi, umpe mambo mengine yanayohusika ili kumuendeleza. Sasa mimi ninahisi hii Mhe. Mwenyekiti, tuangalie na wakati, sisi katika dini yetu tunaelekezwa vile vile kwamba ili kujua kwamba lile ni kosa au ili kujua kwamba pale pana hatari basi tumeambiwa twende katika sehemu fulani tukaangalie. Kwa mfano ili kujua kwamba watu wanapungua katika ulimwengu na watu wanakufa tumeelekezwa twende katika makaburi tukaangalie, tukifika pale tutajua tutapata kuzinduka.

Sasa sheria hii tunasema kila siku tuweke siri tusimtanganze mtu, Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachokijua wale walio na mbwa wakali katika majumba yao au wale wanozitia *fance* zao umeme watangaza, anatangaza kwamba hapa usipite pana mbwa mkali, maana yake nini. Maana yake atakutafuna. Sasa unatakiwa ujuwe kwamba kuna tatizo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili tutalilinda mpaka lini Mhe. Waziri, tutaliweka mpaka lini kwamba watu hawa wasijulikane, hivyo kutokujulikana kwake si kutakakosababisha wengine kuliendea lile jambo.

Mheshimiwa, tunajuwa vijana wetu katika mitaa huko wanashawishika kwa mambo tofauti. Sasa ushawishi huo nikijua kwamba huyo anayenishawishi tayari ana suala fulani basi nitajiepusha nae, lakini keshanipakia kwenye gari

la *PRADO* sijawahi kulipanda, baba yangu hana mama yangu hana ananambia leo twende pahali fulani, simuelewi yule mtu kama moja au mbili, je, nikimridhia si mambo haya yatakuwa yanaendelea.

Sasa pale ndio niliposema mwanzo kwamba hizi ni taratibu zinazotokana na wenzetu *western* wao kwao huko kuwa na *girl* and *boy friend* ni *normal thing*. Lakini kwetu sisi mambo kama hayo hayatakiwi. Sasa mimi ninahisi katika yote hayo njia moja ya kujikinga ni kumjua mwenye tatizo ili kujiepusha naye, lakini leo kila akishajulikana anaambiwa afichwe. Na kama alivyotangulia Mhe. Bikame Yussuf Hamad, huyo ndio na yeye hajaekewa kipengele chochote kinachomlinda kama atafanya tendo kama hilo. Hakuna sheria inayomwambia mtu ambaye atasababisha mwenzake kumpatia virusi basi anatakiwa afanywe moja, mbili, tatu, hakuna.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninahisi hiki kipengele basi tungekiondosha japo sheria ya kimataifa haitaki, lakini kwa wakati tulionao huku kwetu imeshafikia wakati sasa kwamba wanaotambulika na virusi hivi tuekewe kwenye mabango humo njiani, fulani katika mtaa huu nyoka, ili tupate kuwaepuka si hivyo tutakuwa nao pamoja na kwa sababu ni watu wenye uwezo vijana wetu watawaridhia tu hao. Sasa mimi ninahisi Mhe. Mwenyekiti, suala hili la kuweka siri libakie Ulaya, Uingereza na Marekani lakini kwetu Afrika basi liondoshwe moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia mimi mchango wangu hautakuwa mrefu na kwa mnasaba huo ninakushukuru na ninamuomba Mhe. Waziri, yale ambayo nimemwambia yangeleta utata katika dini basi angeyaondoa. Baada ya hayo nitaunga mkono hoja yake. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti na mimi ninakushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii kutoa mawazo yangu katika mswada tulionao mbele yetu. Kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyetujaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema. Mhe. Mwenyekiti pia nichukuwe nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutuletea mswada huu muhimu ambao uko mbele yetu na tunaujadili, nawaomba wajumbe wenzangu tuuchangie na baadae tuupitishe kwa asilimia zote.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na mchango wangu nianze katika sehemu ya pili ukurasa wa 317 wa mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 3 ukurasa wa pili kifungu cha 3(a) naomba ninukuu kama kinavyosomeka, kifungu kinasema "kutoa taarifa za kuyaelimisha makundi yote katika jamii ikijumuisha watu wenye ulemavu kuhusu virusi vya ukimwi, ukijumuisha na njia za maambukizi na namna ya kujikinga na kujisimamia". Mimi kifungu

hiki ninakipongeza sana, lakini kwa ushauri wangu tu ningeomba kwenye kifungu hiki liongezwe neno hapa kujikinga liongezwe neno kupunguza na kusimamia liongezwe hapa. Kwa sababu nia na madhumuni ni kukinga na kupunguza, hatuna uwezo wa kuondoa lakini tukikinga na kupunguza pamoja na kujisimamia basi hili ni jambo zuri.

Lakini vile vile, niseme katika kujikinga na kupunguza kuwe kujihusisha na visababishi vinavyopelekea mtu kupata maambukizo ya virusi au kupata ukimwi kabisa ndio maana ya kujikinga na kupunguza. Kwa vile ili tufikie huko kuna mambo lazima tuyazingatie.

Kwanza virusi unaweza kuvipata au UKIMWI unaweza kuupata kwa mambo mengi sana lakini njia kuu wataalamu wanatueleza ni njia ya kujamiiana. Kama ni njia hio basi natoa ushauri sana tujikinge na mambo ya kujamiiana kusiko salama. Pili, UKIMWI au virusi unaweza kuvipata kwa mambo mbali mbali ikiwamo kutumia vitu vyenye ncha kali, hii unaweza kupata maambukizi ya UKIMWI ambapo mtu katumia kitu kile halafu kenda kutumia mtu mwengine ambae hajaambukizwa basi unaweza ukapata virusi au hatma yake ukapata ukimwi. Tujiepushe sana na mambo haya.

Vile vile, kuchanganya damu na mtu mwenye virusi unaweza kupata ukimwi mambo haya tujiepushe sana. Pia, kumezuka mambo ya vijana wetu katika kutafuta wapenzi wanaweza wakaridhiana katika kufanya tendo la kujamiiana, lakini mmoja akamwambia mimi siwezi kufanya na yeye akamlaghai akamwambia basi tupeane *love* tu. Sasa katika kuchanganya mate yale ya mtu mwenye virusi na aliyekuwa hana virusi inasababisha kupata virusi au hatimae kupata UKIMWI au kupeana denda kwa lugha nyengine hili ni tatizo lazima tujiepushe na mambo hayo.

Vile vile, Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linaweza likasababishwa katika udungaji wa sindano haya makundi hatarishi haya hawa tunaowaita wavuta unga sindano moja inaweza ikatumiwa na watu kumi pengine mtu huyo anavyo virusi au anao ukimwi basi anaweza kusababisha kwa mtu mwengine maambukizi makubwa sana na yakasambaa, kwa hivyo mambo haya tujiepushe nayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika kifungu hicho hicho lakini kifungu (i) naomba nikinukuu, kinasema "kuendesha, kutaribu na kusimamia tafiti zinazohusiana na virusi vya ukimwi na UKIMWI". Ninamuomba Mhe. Waziri, hapa afanye marekebisho au kama vile marekebisho sikuyaona basi liangaliwe hili neno kutaribu silijui maana yake

hili, lakini hapa ningependekeza tu kuendesha na kuratibu au kama lina maana nyengine akija hapa anipe mana iliyokusudiwa, mimi napata shida kidogo kufahamu.

Mheshimiwa katika kupunguza mambo yanayohusiana na kuambukiza virusi vya UKIMWI au UKIMWI wenyewe basi tunapendekeza kusiwe na vilainisho vya kutumia ambapo wanavitumia watu wanaojamiiana wa jinsia moja (wanaume kwa wanaume), hii huko mitaani kutumia vilainisho ni tatizo, tena Mhe. Waziri, awe makini na hili. Kwa sababu wanaona ile njia ni ngumu basi watumie jambo hili na jambo hili limesambaa lazima lifanyiwe uchunguzi wa kina.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kupunguza maambukizi haya basi ninawaomba wanaume wenzangu kujiepusha kufanya mapenzi na wanawake makahaba ambao njia yao si salama kabisa, tujiepushe na mambo hayo tunaweza tukapunguza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu vile vile wanawake nao wajiepushe kufanya ngono zembe na wanaume ambao hawaogopi UKIMWI, wala hawamuogopi Mwenyezi Mungu, tujiepushe akina mama na njia hizi, tutaweza kupunguza matatizo ya maradhi ya UKIMWI. Vile vile, katika kupunguza tujitahidi sana kuwa waaminifu katika ndoa zetu, hatuwezi kuliondoa lakini tutapunguza kwa asilimia kubwa sana. Kwa hivyo, tukiwa waaminifu katika ndoa zetu sisi na familia zetu basi tutaweza kupunguza tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika sehemu hiyo hiyo ya 3(h) naomba nikinukuu kinasema, "kupiga vita unyanyapaa na ubaguzi na taarifa potofu kuhusu virusi vya UKIMWI na UKIMWI . Watu wanaoishi na virusi vya ukimwi na watu walio katika makundi yalio rahisi kuambukizwa na watu walio katika mazingira hatarishi".

Ni kweli wenzetu wanaopata janga hili la kitaifa si vizuri kuwanyanyapaa kwa sababu ni binaadamu kama sisi leo mtu ni mzima na siku nyengine anaweza akafikia hali kama ile lakini ni kuwapa moyo katika mazingira yale walio, lakini tukiwanyanyapaa wakajihisi kama wametengwa kama si binaadamu. Kwa hivyo, hili ni jambo baya.

Vile vile, niseme tu Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kutoa taarifa zilizo potofu. Jambo hili la kutoa taarifa potofu limeshavunja ndoa za watu, biarusi leo keshatiwa *pico* lakini mtu kwa utashi wake tu au kwa rushwa akatoa taarifa zilizokuwa si sahihi, baadhi ya madaktari, na hiyo imeshatokea nchini petu hapa Zanzibar na kwengineko. Kuvunja ndoa za watu akamtangaza sio

uchunguzi aliopata. Na vile vile, ishatokea kufanya hatarishi mtu amegundulikana akaambiwa hana, akapewa ripoti ambayo si sahihi na kumhatarishia mtu mwengine maisha yake. Mheshimiwa, hapa lazima tuwaelimishe madaktari wetu waliopewa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea na mchango wangu katika sehemu hiyo ya tatu kifungu cha 3 pia ninakuomba kwa heshima kubwa nikinukuu.

> "Katika kuendesha kampeni za elimu na taarifa zilizoelezwa katika kifungu hiki. Tume itashirikiana na wadau husika wa umma, jumiya zisizokuwa za kiserikali, jumuiya za kijamii na sekta binafsi na kuhakikisha uhusishaji na ushiriki unaofaa wa makundi yote ya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi'

Mimi kifungu hiki ninakipongeza mia juu ya mia katika kuzishirikisha taasisi ambazo zisizokuwa za kiserikali na ni jambo jema kuwaelimisha. Lakini katika kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika ukurasa wa 319 Sehemu ya Tatu vile vile imezungumzwa taarifa na elimu ilikuwa katika kifungu cha 5(e) kwamba ifanyike katika na taasisi nyengine za elimu, Chuo cha Mafunzo na Kizuizini au katika sehemu za ibada, sehemu ya kazi, polisi na vikosi vya ulinzi mjini na vijijini.

Hii ni nzuri katika kutoa elimu, lakini Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba waziri kasahau katika kundi moja muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, katika makundi ya wavuvi ambao wanakwenda dago basi elimu hii ingetolewa zaidi kwa sababu watu hao wanakaa muda mrefu na kama hawakupata elimu hii wanaweza kuleta hatari ya mambukizo. Naomba kipengele hiki liongezewe.

Halafu katika zile jumuiya basi watu wanao-*deal* na wavuvi kwa mfano, Kojani iko Jumuiya ya Kojani *Fishermen Development Organization* (KOFIDO) hawa wakipewa uwezo katika kuelimisha nao watasaidia kwa sababu ndio wanao-*deal* na wavuvi walio wengi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 329 kifungu cha 24(1) naomba ninukuu.

Kifungu 24(1) kinasema kwamba,

> “Kila mtu anastahiki faragha na kufichiwa siri kuhusiana na hali yake ya UKIMWI”

Mhe. Mwenyekiti, si vibaya kufanya siri kwa jambo hili, lakini kinadharia jambo hili ukilifanya siri sana basi linaweza kuwaumiza wengine waliokuwa

hawajapata maambukizo ya UKIMWI. Tunapata tetesi kama wengine wakishajitambua na ana uwezo basi anatumia uwezo wake wa kifedha kuwarubuni wengine kuwapa maambukizo kama hayo, hata akijulikana kama anaambukiza ameshawasaliti wengi. Basi tunashauri Mhe. Mwenyekiti, pamoja na siri iliyopo ni bora watu kujulikana ili wengine wapate kinga. Unapokwenda sehemu kama pana hatari kama mbwa mkali basi wewe mwenyewe utafanya tahadhati, lakini kama hujui basi unaweza kumvamia.

Mhe. Mwenyekiti, tumezowea mtu mwenye UKIMWI ni mtu mwenye kuwa mwembamba tu, lakini siku hizi basi hao walioathirika ni wanene zaidi kuliko sisi, humjui ni nani na anapendeza kweli kweli. Kwa hivyo, hili ni tatizo na lazima tuwajue, sheria iweke bayana tuwajue ili tujikinge.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa haya machache naunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa kuchangia mswada huu unaohusiana na UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu ni mdogo tu. Kwa leo nachangia kifungu cha 5(1) kinachosema kwamba Tume itatoa elimu kwa wananchi kuhusu chanzo, sababu, njia za maambukizi, athari na mbinu za kujikinga na UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, kinga ya UKIMWI kwa sisi Wazanzibari hivi sasa kwa takwimu kubwa inasemekana kwamba tumeathirika sana. Mimi mchango wangu ili kunusuru wananchi wa Zanzibar naishauri serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwamba itoe elimu hasa katika taasisi za kazi, vyombo vya habari navyo vitumike kwa kuelimisha wananchi na hasa kuangalia sehemu za mikusanyiko. Kwa mfano sasa hivi tuna sehemu za bandari nyingi sana, tuna sehemu kama viwanja vya ndege, na Bandari kuu Malindi pale.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu hapo hapo ni kwamba serikali ichapishe vitabu kuwaenezea wananchi ili kuelimika na janga la UKIMWI, tukipata vitabu wengi wetu tutasoma na tutatambua. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae amenijaalia kuwepo katika kikao hiki nikiwa mzima na afya njema. Lakini pia nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuwa miongoni mwa wachangiaji mswada huu ambao ni muhimu sana kwa taifa letu.

Lakini vile vile, nichukue nafasi hii ya dhati kabisa kumshukuru Mhe. Waziri, mwanamama mwenzetu, mwanamama mahiri kwa kuleta mswada huu ambao ninaamini kwamba kama utafanyiwa kazi ipasavyo basi mambo mengi yatatupungukia katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wamechangia suala la UKIMWI kwa kweli ni suala kubwa, ni janga kubwa katika taifa letu na niseme kwamba janga hili linaweza likamkumba mtu yeyote. Kwa hivyo, niseme kwamba namshukuru sana Mhe. Waziri, lakini lazima tukubali kwamba kuna kazi kubwa mbele yetu ya kuhakikisha kwamba mbali ya haya tuliyoletewa lakini kuhakikisha kuwa tunapunguza tatizo hili kubwa la maambukizo ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, kikubwa zaidi tunaweza tukasema kuwa hili tatizo kwa asilimia kubwa sasa hivi limeweza kupatiwa ufumbuzi, lakini pia, kwa sasa hivi kuna maradhi mengine makubwa yanauwa kwa haraka sana kuliko suala la UKIMWI. Kuna maradhi ya kensa, shindikizo la damu ambayo bado hayajapatiwa dawa. Lakini suala la UKIMWI kama utajitambua mwenyewe na kama utafuata miko ambayo umewekewa basi tunao humu tunatembea nao mtu ana-*survive* miaka 20 mpaka 30 na kama utaambiwa huyu ameathirika unaweza ukakataa.

Kwa hivyo, labda mimi nitoe wito kwa jamii baadhi ya wenzetu pengine unapokwenda kupima tu ukagundulikana tayari umeathirika tunachanganyikiwa. Kwa kweli tusichanganyikiwe, kwa sababau unapochanganyikiwa unajipunguzia umri wako wa kuishi.

Kwa hivyo, lazima tukubali suala hili lakini pia tusiliogope, kwa sababu kuna wengine *physiological* anapokwenda kupima UKIMWI akagunduliwa tayari ameathirika kwa kweli akitoka pale hospitali mgonjwa kitandani, hata zile *CD4* hazijashuka lakini lile suala la kuambiwa wewe sasa hivi umeshaathirika na gonjwa la UKIMWI mtu anakata tamaa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu labda nimwambie tu Mhe. Waziri kuwa pamoja na kuyazungumza haya ambayo yamezungumzwa katika mswada huu, lakini lazima tukubali Mhe. Waziri, kwamba kama hatujawa tayari kuhakikisha kwamba tunadhibiti madawa ya kulevya kwa kweli suala hili la UKIMWI tutakuwa hatujalipunguza.

Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya yanachangia kwa kiasi kikubwa mno katika maambukizi haya ya UKIMWI na sote tunafahamu. Kwa kweli sasa hivi watumiaji wengi wa madawa ya kulevya wanajidunga sindano na sote tunafahamu kwamba sindano ni tatizo ambalo linapelekea uambukizaji wa maradhi haya ya UKIMWI.

Lakini sio hilo tu Mhe. Mwenyekiti, tatizo hili la uambukizaji kwa sindano tunafahamu sote vijana wetu wanakaa katika majumba mabovu, wanajidunga sindano na baada ya kujidunga sindano zile wanatupa mabomba ovyo na kupelekea watoto wetu ambao wanacheza katika majumba yale wanaokota na kuchezea. Kwa hivyo, na wao wanakumbana na mazingira hatarishi kupata uambukizaji wa UKIMWI.

Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakuomba tuliangalie hili. Sio tu Mhe. Mwenyekiti, pia nimwambie Mhe. Waziri, na hawa wanaojidunga wakati mwengine mtu muathirika anajijua yeye ana tatizo hili anampa mwenzake bomba lile kwa makusudi ajichome ili na yeye awe muathirika. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, nilikuwa natoa angalizo kwa serikali yetu.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, niingie katika mswada wenyewe, nije katika ukurasa wa kwanza ambao unazungumzia suala la muathirika. Imesemwa hapa mtu muathirika maana yake ni anahusiana au anayeshirikiana na mtu mwenye au anaeaminika kuwa anaishi na Virusi vya UKIMWI, au mwenye au anaaminika kuwa ni mwanachama au anayeshirikiana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli imezungumzwa kwa kirefu hapa lakini mimi kwa muono wangu naona sipati mantiki sahihi. Kwa sababu tukisema maana ya muathirika kuwa mtu anaehusiana basi sote humu tayari tumeshaathirika, kwa sababu tumo tunahusiana, ama mtu jamaa yako, lakini pia anaeshirikiana, kushirikiana sote humu Mhe. Mwenyekiti, tunashirikiana, pengine mtu aliekuwa nje huko pia wanashirikiana.

Sasa mimi naamini kwamba mtu ambaye ameathirika ni yule ambae amepima na akapata cheti cha daktari kuwa yeye tayari ameathirika na ugonjwa huu wa UKIMWI. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, atapokuja anieleweshe ili nifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika ukurasa wa 327, pamezungumzwa kipengele cha pili kuwa, bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kijifungu cha (1) cha kifungu hiki hakutatakiwa ridhaa kwa mtu kupima Virusi vya UKIMWI ikiwa labda kwa amri ya Mahakama katika kuchangia viungo na vitu vingine vya binadamu, kwa watuhumiwa wa makosa ya kujamiiana na kwa wanawake wajawazito.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona kama waziri pengine kasahau suala moja ambalo ni la msingi kabisa, angeliongeza kikawa kifungu (e) kwamba na wanandoa nao ni lazima wapime. Kwa sababu sasa hivi makadhi wamehamasika kuwa hawaozeshi mpaka waone cheti cha hospitali lakini haimo kisheria, kwa hivyo mtu ana hiari yake. Pia, hii inaweza kutoa fursa

kwa watu wenye maabukizo kufunga ndoa bila ya kupima, pengine mtu anatoka mbali kama Dar es Salaam au hapa hapa Zanzibar, lakini hajuilikani!

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika suala zima la ulinzi, ukurasa wa 329, unasema ulinzi wa jumla wa haki za mtu anaeishi au alieathirika na virusi vya UKIMWI. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo ni zuri sana mimi nimpongeze Mhe. Waziri, lakini niseme kwamba hii haki ya kumlinda huyu mtu aliyeathirika sio yake peke yake, mimi nadhani na huyu mtu ambaye hajaathirika na yeye ana haki zake za kulindwa na haijaoneshwa katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wengine kwa makusudi au bila ya kukusudia mtu tayari ameathirika anaweza akachukua kiwembe akakata kucha pengine kucha ile akatoka damu, sasa baada ya kuchukua kiwembe kile akakichimbia shimo akafukia ili mtoto asije akachezea mtu yule pengine anatupa kwa makusudi na sehemu ile labda kuna watoto.

Sio hivyo tu Mhe. Mwenyekiti, kuna watu pengine tayari mtu anajua ameathirika anamfuata mtu kwa kimapenzi, lakini kutokana na ile akili yake anaijua mwenyewe anamfuata mtu ambaye yeye hajaathirika na anamlaghai kimapenzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende katika ukurasa wa 331, tumeoneshwa hapa mfanyakazi ambae anaishi na virusi vya UKIMWI ambae anafanyia kazi sehemu fulani, lakini pengine kutokana na yale matatizo aliyonayo sehemu ile haimfai tena kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tungeweka rasmi kwamba labda mtu alikuwa anafanya kazi katika eneo hili lakini kutokana na sababu ya zile kazi zenyewe pengine mtu anashikashika vitu ambavyo vinaweza vikamchinja, sasa mtu kama yule hapa pengine patakuwa hapamfai tena, basi iweko kwamba mtu yule anaweza akabadilishiwa eneo la kazi akawekwa eneo jengine ambalo sio hatarishi. Kwa sababu naona katika mswada huu haujaonesha suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, labda nimalizie mchango wangu kama nilivyosema kwamba mchango wangu hautakuwa mkubwa. Katika ukurasa wa 318 pamezungumziwa suala zima la mambo ya mila na desturi. Mhe. Mwenyekiti, hizi mila potofu kwa sababu unaweza ukasema kwamba mila hii potofu lakini pengine kwa yule aliekuwa mila yake, yeye anaona si potofu. Kwa hivyo kama tutazungumza moja kwa moja kwamba kufanya kwa mila potofu mimi nadhani Mhe. Waziri nimwambie tungeweka vizuri tu kwamba mila ambazo zitakuwa hazistahiki katika kidini. Kwa mfano labda suala zima la ukeketaji

nafikiri tungeweka wazi hapa unasababisha uambukizi wa maradhi ya UKIMWI, lakini pia mila nyengine kwa Kiswahili wanaita kutahiri. Kwa hiyo, hapa mimi naona ingeoneshwa bayana, isingesemwa hii mila potofu, kwa sababu kila mtu na mila na desturi zake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametuwezesha kutufikisha siku hii ya leo katika hali ya uzima ili kujenga taifa letu. Lakini pia, nichukue nafasi hii na mimi nijumuike na wenzangu nipongeze kwamba leo ule mfumo dume umeondoka, leo tuna Mwenyekiti Mwanamke na makatibu wetu wote ni wanawake, inaonesha kwamba mfumo dume sasa tunaukata kidogo kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nimpongeze sana Mhe. Waziri ambae ameleta marekebisho ya mswada huu ili kuona kwamba taifa hili baadae litakuwa ni taifa ambalo halina watu ambao wanaweza kusaidiwa hapa na pale. Lakini mimi niseme tu kwamba tusijidanganye kwa sababu UKIMWI ni tatizo sugu na ni tatizo kubwa kwa ulimwengu mzima, tukiacha wenzetu huko nje wenye madawa mbali mbali, lakini sisi unatuathiri vibaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe sana wizara ambayo inashughulikia masuala haya, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini pia ishirikiane na Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, nieleze kwamba tusijidanganye hali halisi inayozungumzwa kwa virusi vya UKIMWI ambayo imeshatuathiri ni kubwa. Mimi naweza kusema ni kubwa kwa sababu wale ambao wanakwenda hospitali ndio wanaojulikana. Lakini kuna wengi sana ambao kwa kuhofia nafsi zao au kwamba atanyanyapaliwa haendi hospitali, na kuna watu wanajijua.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe wizara husika pamoja na Wizara ya Afya kwa sababu wizara hizi lazima ziende sambamba. Tuhakikishe mswada huu unafanyiwa kazi, yale mapendekezo ambayo tunayatoa basi yanafanyiwa kazi vizuri sana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nimeingiwa na hofu sasa hivi, nimeingiwa na hofu kutokana na unyanyasaji ulioingia, watu wanakwepa kwenda kupima na hatimae kuwaangamiza vijana wetu watoto kuanzia miaka mitatu, minne mpaka kufikia kumi na kuendelea ni kutokana na suala hili.

Ninatoa wito Mhe. Mwenyekiti, watu hawa ni hatari kwa sababu anajua anakwenda kijana ambaye anajua huyu hana ukimwi na yameshatokezea Mhe. Mwenyekiti. Mtoto wa miaka minne amepimwa kumgusa tu, akaonekana ana ukimwi. Kwa hivyo, naomba wananchi suala hili tulizingatie na tulitilie maanani kwa ajili tutaua vijana wetu ambao hawana hatia, hawajui kusi wala kaskazi.

Lakini pia, Mhe. Mwenyekiti, niunge mkono maneno aliyoyazungumza msemaji aliyekaa kitako Mhe. Amina Iddi Mabrouk, kwamba ni vyema hizi ndoa sasa hivi basi mume na mke wakapime na wasipime kila mtu kwake, kama kuna ndoa wafuatane hawa watu wawili waende wakapime kila mmoja amuone mwenziwe.

Ninajua hapa mambo mengi kwa sababu hili la ukimwi tutatumia haki za binadamu. Lakini haki hizo za binadamu na yule aliyekuwa hana ukimwi naye ana haki ya kulindwa kwa mtu ambaye anajijua ana ukimwi, lakini anafanya kwa makusudi. Kwa hivyo, mimi ninadhani Mhe. Waziri, hapa apime aweke mezani sawa, kwa sababu kila mtu ana haki yake katika taifa lake.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba sasa hivi hawa wagonjwa wa ukimwi kwanza niwape pole kwa sababu tusiseme kajitakia, hakujitakia ndio ulimwengu ulivyo, wala tusiwacheke ni kuwapa pole na wala tusiwanyanyapae. Lakini sasa taratibu zimuweke pazuri yule ambaye ana maradhi ya ukimwi.

Niseme wenzangu tujitahadhari kwa sababu wanamtizama mtu ambaye wana hakika wameanza kuingia kwa watoto, sasa hivi wanasema watu wazima mwenye umri ambaye anajua huyu hana ukimwi. Anatoka mtoto mdogo kabisa ambaye si kiasi, lakini anamlaghai mama mtu mzima yule kuona kwamba atimize haja zake.

Nitoe wito tu Mhe. Mwenyekiti, jamani hili suala si la kulifanyia masikhara. Suala hili huo ugonjwa wenyewe umekaa pabaya. Kwa hivyo, ni lazima tuwe na tahadhari na kubwa zaidi ni kujikinga na zinaa. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kujikinga ndio suala ambalo litaweza kutusaidia. Lakini niunge mkono kwamba ugonjwa wa ukimwi unakwenda sambamba na madawa ya kulevya. Hivyo, niseme tu kwamba kwa sababu madawa ya kulevya pia yapo katika ofisi hii hii, wakae waitafakari sheria hii kila mmoja apewe haki yake.
Na mimi nilisema nizungumze hayo na nitoe tena tahadhari kwa watoto wetu wanaume ambao ni wadogo na watoto wetu wanawake ambao ni wadogo. Ninasema tena ambayo itakuwa mara ya tatu au nne, lazima kuna mtandao unafanya kwa makusudi.

Ninaiomba serikali ihakikishe inakwenda chini kabisa kuangalia ni kitu gani kilichosababisha masuala haya ya vijana wetu ambao wanatendewa mambo ambayo si mazuri.

Baada ya kusema hayo kwa sababu na mimi ni mzazi, niliona si vyema kama mswada huu nisingeuchangia. Kwa hivyo, baada ya kusema hayo niseme na mimi niunga mkono moja kwa moja na tuombe Mwenyezi Mungu atuondolee janga hili la ukimwi kila siku zijazo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Asha Bakari Makame, anafuata Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadae atamalizia Mhe. Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na mchana huu tukiwa tunaendelea na shughuli za kuwakilisha wananchi wa Zanzibar katika chombo chao hiki muhimu.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kuniona pamoja na kwamba nimekuletea taarifa punde tu ya kukuomba kuchangia na mimi ukanipa fursa nieleze machache kuhusiana na mswada huu.

Tatu, Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, kwa kuwasilisha kwake mswada huu muhimu sana katika kulinda afya za wananchi wetu, lakini pia katika kulinda haki za wananchi wote bila ya kujali hata wale ambao wameathirika na maradhi.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni muhimu sana, umuhimu wake umeelezwa katika maelezo yaliomo katika mswada kwenye madhumuni na sababu kwamba lengo lake moja ni kuondosha mkorogano wa aina fulani ambao hivi sasa upo katika utekelezaji wa masuala mbali mbali ya mapambano dhidi ya ukimwi kwa sababu ya kuwepo sheria na kanuni mbali mbali ambazo pengine nyengine zinapizana, lakini na vile vile kutokana na kazi ambazo zinafanywa na serikali na jumuiya au taasisi ambazo si za kiserikali katika suala hili ambalo linakosa pahala pa kuratibiwa moja kwa moja.

Kwa hivyo, tunavyoambiwa mswada huu ukipita na baadae Mhe. Rais akiukubali unategemewa uweze kuondosha mgorogano huo uliokuwepo. Kwa hivyo, ni mswada muhimu sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa sababu hiyo Mhe.

Mwenyekiti, ninadhani ni muhimu kila kitu katika mswada huu kikawa wazi na kinachoeleweka vizuri.

Kwa hivyo, kwanza ningependa niungane na wenzangu ambao wametaka ufafanuzi kidogo katika tafsiri ya baadhi ya maneno. Na mimi ningemuomba Mhe. Waziri, pia, akatusaidia kwamba, je, hii tafsiri ya neno "mtu aliyeathirika" ni tafsiri sahihi. Kwa sababu hapa katika mswada imeandikwa kifungu cha 2 Mhe. Mwenyekiti, "mtu aliyeathirika kuhusiana na virusi vya ukimwi (*VVU*) na ukimwi inajumuisha mtu ambaye:-

a) Anahusiana au anashirikiana na mtu mwenye au anayeaminika kuwa anaishi na virusi vya ukimwi.

b) Mwenye au anayeaminika kuwa ni mwanachama anashirikiana na kikundi, harakati au anafanya kazi au anaishi katika mazingira ambayo hayahusiki au yanaaminika kuwa yanahusika na madhara au yanaambatana na uenezaji au ueneaji wa ukimwi".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hata ukiangalia katika mswada wa Kiingereza maneno yaliyotumika ni, maana yake ni hiyo hiyo, maana yake mwanzo nilidhani labda kuna tatizo la tafsiri. Sasa ninataka kumuuliza Mhe. Waziri aje atusaidie Mhe. Mwenyekiti, kwamba, je, tafsiri hii ni sahihi kwamba tunamuhesabu mtu hata anayehusiana au anayeshirikiana kwa Kiingereza maneno yaliyotumika *"is related to or with as associate with"* na mtu ambaye ana ukimwi naye anatafsirika kwamba ni mtu aliyeathirika.

Lakini vile vile, kwamba mtu ambaye anaaminika kuwa mwanachama au anashirikiana na kikundi tu au wanafanya harakati, wanafanya kazi au anaishi katika mazingira ambayo yanayohusika na masuala haya atatafsirika kwamba na yeye vile vile ameathirika. Ninajiuliza Mhe. Mwenyekiti, kwamba kwa tafsiri hii ikiwa tutaikubali hatutofanya kinyume na madhumuni ya mswada huu.

Madhumuni ya mswada ni kuweka mazingira mazuri, lakini ninaogopa kwamba ikiwa tafsiri itabaki hivi wanawezekana watu ambao hawana ukimwi, hawana virusi vya ukimwi, lakini wanasaidia harakati za kupambana na ukimwi, wanawasaidia wale walioathirika wakajiondosha tu kwa sababu tu kwamba kuendelea kushiriki kwao kutafanya na wao watafsirike kwamba na wao vile vile ni waathirika. Na kama tunavyojua bado tunaishi, jamii mambo haya yanaleta tafsiri mbaya, yanaleta mara nyengine kutengwa, madhumuni ya mswada yameondoa haya, lakini bado yapo.

Sasa, je, wale watu kwa mfano wanaoshirikiana na jumuiya kama *ZAPHA plus*, tunawaambia au tunawapelekea ujumbe kwamba wasishirikiane tena kwa sababu kushirikiana nao, maana yake wewe tena unahesabika kwamba ni muathirika. Nilikuwa ninamuomba hilo Mhe. Waziri, atuweke sawa ili tuone kama kweli tunahitaji kubakia katika tafsiri hii.

Eneo la pili, ambalo nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija anisaidie Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi ni tafsiri ya maneno ambayo yapo katika ukurasa 315 juu kabisa pale, "Mambo yanayohusiana na haki za binadamu'. Imetafsiriwa maana yake ni mambo yote yanayohusiana na mambo ya binadamu kama yalivyoainishwa katika ibara ya 11 ya Katiba ya Zanzibar 1984.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ni katika Katiba ambazo zinapigiwa mfano katika masuala ya haki za binadamu. Zanzibar imejijengea sifa katika hili kwamba hata wenzetu Jamhuri ya Muungano mwaka 1984 hawakulitaka hili, lakini walilazimika kuliingiza katika Katiba kwa sababu Zanzibar imeng'ang'ania kwamba Katiba yake lazima kuwepo na *bills of right*, yaani eneo au sura ya Katiba ambayo inayohusiana na haki za binadamu.

Sasa nimepata tabu kwamba mswada huu lengo lake ni kulinda haki za watu, lakini kwa nini katika tafsiri tumeupelekea unatafsirika kwamba kwa madhumuni yake ni kifungu cha 11 tu cha Katiba. Kwa sababu katika Katiba yetu kuna sura nzima inayohusu kinga, haki za lazima, wajibu na uhuru wa mtu binafsi ambao ni kuanzia kifungu cha 11 hadi kifungu cha 25 (a).

Kwa hivyo, nilikuwa ninadhani kwamba ku-*restrict* kudogosha tafsiri ya haki za binadamu mpaka kusema inahusu kwamba kifungu cha 11 tu ambacho ni kifungu moja, kwamba hili suala si sahihi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba pia hili Mhe. Waziri, akija atusaidie.

Mhe.Mwenyekiti, nikiondoka katika ufafanuzi, maeneo mengine ambayo ningependa niyachangie kwa ufupi. Moja linahusu sehemu ya kwanza, lakini zaidi sehemu ya sita ya mswada huu, kifungu cha 23 hadi 31 ambavyo vinazungumzia haki za waathirika au wanaoaminiwa kwamba wameathirika.
Mhe. Mwenyekiti, sina mchango mahususi juu ya namna ya kubadilisha vifungu. Vifungu vimekaa vizuri tu kwa mtizamo wangu, lakini ninachokihofia ni kile ambacho kimeelezwa na Mhe. Mwakilishi, mwenzangu Asha Bakari Makame. Mhe. Asha Bakari Makame alipokuwa anachangia punde hivi kasema kwamba katika kulinda haki za binadamu za watu walioathirika, isije ikatufikisha pahala tukaathiri haki za watu ambao hawajaathirika bado.

Sasa ninasisitiza kwamba ni vizuri kulinda haki hizi ambazo zimetajwa katika kifungu cha 23 hadi 31 cha mswada huu, lakini naomba itakapokuja utekelezaji tusimamie katika njia ambayo pia tutahakikisha kwamba tunalinda afya, moja katika haki ya binadamu ni kulinda afya za watu vile vile. Kwa hivyo, tunawalinda wale ambao hawakuathirika bado, isije ikawa tuna-*emphasize*, tunasisitiza mno katika haki za waliokuwa wameathirika, ikaja ikaingiliana na kuja kupelekea kwamba wanalindwa kiasi ambacho wameweza kufanya vitendo ambavyo vinapelekea kuathiri wengine.

Na Mhe. Mwenyekiti, haya yapo, tunaishi katika jamii hizi hizi, tunasikia matukio ambayo watu anajijua ana ukimwi anakwenda kufanya mambo makusudi kueneza ukimwi, ni kama vile anahisi kama kakomolewa na yeye anakomoa watu, wakati ni mambo ambayo yanayoweza kutokezea kutokana na mazingira tofauti, kama ilivyoelezwa wala si lazima kwamba umeupata ukimwi kutokana na vitendo vya kujamiana tu, hapana. Tumeelezwa kuna njia nyingi unaweza ukapata ukimwi.

Unaweza pengine ukamchangia mtu damu tu au pengine umekwenda kutoa damu umedungwa sindano, kuna mambo mengi yanayopelekea ukapata ukimwi. Sasa ninahofia kwamba tunapowalinda hawa isije ikapelekea vile vile kuja kuathiri wengine. Kwa hivyo, ni muhimu hilo likazingatiwa.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ninataka kukizungumzia kifungu cha 9 cha mswada katika sehemu ya tatu. Hapa sehemu ya tatu kunazungumziwa "Taarifa, elimu na mawasiliano kuhusu virusi vya ukimwi na ukimwi".

Kifungu cha 9 kinazungumzia jukumu la vyombo vya habari katika kutoa elimu. Sasa hapa mimi ninataka kumwambia Mhe. Waziri, na serikali kwa ujumla, haya yaliyokuwepo hapa mimi sina matatizo nayo katika kutumika vyombo vya habari kutoa elimu na mawasiliano juu ya masuala ya ukimwi, lakini je, upande mwengine tutachukua hatua kiasi gani kuvidhibiti vyombo vya habari visitangaze vipindi au kuonesha mambo ambayo yanayopelekea vishawishi vinavyopelekea kuenea kwa ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, katika jamii yetu hivi sasa chini ya msingi wa mfumo wa soko huria, mara nyengine inatumika vibaya tafsiri yake kwamba hakuna tena kusimamia maadili wala udhibiti, si kweli. Hakuna jamii hata moja ambayo haichungi maadili. Sasa nilikuwa ninasema ni muhimu sana kuona kwamba vyombo vya habari vinavyomilikiwa na serikali kwa maana ya vyombo vya habari vya umma lakini hata vya binafsi.

Vile vile, kuna haja ya kuvichunguza, kuvifuatilia na kuvisimamia, wasiwe wanarusha vipindi hewani ambavyo badala ya kutukinga dhidi ya ukimwi, vikawa vyenyewe vinapelekea kutoa vishawishi katika kukiuka maadili na hivyo kupelekea kusambaa kwa ukimwi. Ninadhani hilo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri alitazame sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu hiyo hiyo ya tatu ni kifungu cha 6. Hapa ndio nina wasi wasi sana Mhe. Mwenyekiti. Hiki kifungu cha 6 kipo ukurasa wa 320 pale juu, kinazungumzia, "elimu ya virusi vya ukimwi na ukimwi katika taasisi za elimu", na kinatoa jukumu maalum kwa Wizara inayohusika na elimu kusimamia suala hili.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, jamii yetu ina maadili yake na jamii yoyote yenye ustaarabu mkongwe kama ilivyo jamii ya Kizanzibari inajifaharisha na maadili yake. Mara nyengine tunafanya mambo ambayo tunadhani kwamba inapelekea kutukinga, lakini inaweza ikawa madhara yake ni kueneza.

Mhe. Mwenyekiti, ulikuwepo katika semina ya Wawakilishi tuliyofanya kule *Coconut Beach*. Katika kuonesha kwa vitendo jinsi ya kutumia zana fulani hizi, kwa mtu mzima anayejua kutumia mambo yale pengine akifahamisha namna uzuri zaidi ya kutumia ili kujikinga ni suala jengine, lakini kwa wanafunzi ambao ni vijana wadogo, pengine moja kinachompelekea kutojiingiza katika vitendo vya uasharati au kujamiana au vitendo vyengine vyovyote vinavyokwenda kinyume na maadili yetu, ni kwamba anahofia pengine kushika uja uzito na mambo mengine kama hayo na pengine kwa mambo ya jamii yetu hawajui kutumia mambo kama yale, haidhuru tunaambiwa siku hizi jamii imebadilika wanajua wote, si kweli si wote. Inawezekana pengine katika maeneo ya mijini mambo yapo, lakini bado kuna maeneo mengine yanalindwa.

Lakini unapoichukua elimu hii na elimu hii Mhe. Mwenyekiti, ikiwa madhumuni ya kifungu cha 6 ni kwenda kutoa elimu kama ile tuliyooneshwa sisi *Coconut Beach* kwenda ikapelekwa katika maskuli, ile itakuwa hatukingi tunakwenda kueneza ukimwi maskulini. Vijana ni vijana tu, wana *element* ya kuchukua *risk* tu ya kutokujali matokeo ya mambo. Kwa hivyo, unapomuonesha dogo, atafanya kubwa tu Mhe. Mwenyekiti.

Ndio yale yanayozungumzwa, Waswahili wanasema, "utampa shubiri atachukua pima". Sasa mimi ninaliogopa sana na Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi mimi ninatahadharisha kwamba mara nyengine kuchukua sheria tukazitunga kama tunavyoletewa kwa kukopia sheria za nchi nyengine ni matatizo. Kila jamii ina mazingira yake, utamaduni wake, silka zake na maadili yake.

Katika jamii zetu haya mambo mengine kuwa na uwazi kama huu inawezekana Mhe. Mwenyekiti, inakubalika katika jamii za huko, katika jamii zetu ni ngumu. Lakini kwa maelezo ya kifungu cha 6 nilikuwa Mhe. Waziri, anitosheleze hasa kwamba utekelezaji wa kifungu hiki hautopelekea kuwapelekea wanafunzi wetu kuwaingiza katika mambo ambayo pengine hatuafiki.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, naomba nikichangie kidogo kifungu cha 10 ambacho kinazungumzia, "taarifa na elimu ya virusi vya ukimwi na ukimwi katika jamii". Hapa kimetajwa vile vile viongozi wa kidini. Ninaunga mkono kikamilifu kuwashirikisha viongozi wa kidini katika mapambano dhidi ya ukimwi.

Na moja ambalo mimi Mhe. Mwenyekiti, ninalonivutia katika miji yetu mbali mbali na hata vijiji ukenda, ninapoona yale mabango ambayo yanaashiria kutoa elimu ya kupambana na ukimwi badala ya kutoa elimu kuhusu kutumia mambo yaliyokuwa hayakubadiliki. Wanasema wanakataza ukimwi kwa kutumia maadili yetu kwa kutumia elimu ya kidini kwamba athari ya vitendo hivyo isifanywe. Imeenezwa kwa uzuri sana.

Sasa kwa hivyo, inaonesha umuhimu wa kutumia viongozi wa kidini, lakini na mimi nitahadharishe tu isije ikawa hii ingawa kifungu kimekaa vizuri hakishurutishi jambo lolote, isije kikatumika Mhe. Mwenyekiti, kupelekea kuwataka viongozi wa kidini kwamba lazima akatoe elimu fulani ambayo pengine haikubaliani na mafunzo ya kidini katika jamii zetu na kwa hili kwa dini zote, nilikuwa naomba kusisitiza hilo. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo, naomba pia nizungumzie tahadhari. Kama nilivyokwisha eneo la kifungu cha 35. Hiki kipo katika sehemu ya saba inayozungumzia haya makundi yanayoitwa hatarishi. Lakini nimeamua kukizungumzia kifungu cha 35 makusudi, ninajua watoto, wanawake wasichana, matokeo ya ubakaji yamekuwa yanazidi na walemavu yote yanazungumzwa haya.

Lakini kumetajwa habari ya wafungwa. Katika tafiti nyingi zilizofanywa Mhe. Mwenyekiti, imeonesha katika maeneo kunakuwa na uambukizaji mkubwa, ni katika magereza au kwa kwetu ni vyuo vya mafunzo. Kwa sababu kule binadamu anaishi katika hali ambayo ana tafrani nyingi. Mara nyingi kunakuwa na njia ya kujisaidia watu wanafanya vitendo vilivyokuwa hata havikubaliki katika maisha ya binadamu.

Sasa nilikuwa ninadhani kwamba katika utekelezaji kuna haja, lakini kifungu hiki kilikuwa na dhamira nzuri kifungu cha 35, kitakuwa hakitekelezeki kama

wizara hii haikupata ushirikiano wa kutosha kutokana na Chuo cha Mafunzo chenyewe na uongozi wake. Mambo mengi kule yanaachiwa wazi mno kiasi ambacho vinafanyika vitendo ambavyo havikubaliki.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla, siku moja alitwambia hapa Mwakilishi wa Jimbo la Chonga, kwamba alikuwepo kule katika mazingira ya siku za nyuma, kashuhudia mambo ambayo huwezi kuamini kwamba yanafanyika katika Vyuo vyetu vya Mafunzo. Kwa hivyo, ninasema kifungu kizuri na malengo yake mazuri, lakini utekelezaji wake ili ufanikiwe, unategemea mashirikiano makubwa kutokana na uongozi wa Vyuo vya Mafunzo. Kwa hivyo, nilikuwa ninasisitiza kwamba hili tulitizame sana.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo mawili ya mwisho. Kwanza kifungu cha 36, lakini hasa nikikihusisha na kifungu cha 39. Hapa kifungu cha 36 kinazungumzia, "Utafiti na majaribio ya tiba", lakini kifungu cha 39 kinazungumzia, "Taarifa za kupotosha".

Sasa mimi ninazungumzia hizi taarifa za kupotosha. Kifungu kinasema Mhe. Mwenyekiti,

> "Mtu hatotoa au kupeleka taarifa au jambo lolote au kupeleka taarifa zinazohusiana na matibabu ya virusi vya ukimwi isipokuwa kama taarifa ipo sahihi na imethibitishwa kisayansi,(2) Taarifa inayokusudiwa ya matibabu ya virusi vya ukimwi kwa mujibu wa kifungu cha 1 cha kifungu hiki itaambatanishwa na ushahidi wa kisayansi wa matokeo ya kabla na baada ya kupima,(3) Mtu atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa"

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ilikuwa na maadili yake mazuri sana, ustaarabu wake mkongwe, lakini maingiliano ya jamii yamezidi. Imekuwa sasa baadhi ya mila ambazo hatujazizoea sisi zinakuja, unakuta kuna mganga au mutanisamehe sina nia ya kutaja mtu fulani labda kwa kabila lake, ndugu zetu wa Kimasai anakuwekea tangazo ana mambo anatibu unaorodheshewa pamoja na ukimwi. Tunayaona Mhe. Mwenyekiti, katika Zanzibar hii hii.

Wakati fulani nilikuwa Darajani pale katika eneo la soko kuu mpaka kwenye makontena unayaona matangazo haya. Sasa ninajiuliza kwamba dunia nzima inatafuta, kama ingekuwa huyu kweli ana dawa hii si angekuwa ameshapata ashakuwa milionea. Lakini ninajiuliza mamlaka za serikali zinakuwepo wapi mpaka zinaachia mtu anabandika matangazo kama yale. Wala mimi siamini kama kunahitajika kuwe na sheria hii ndio suala hili lichukuliwe hatua, kwa

sababu haya mambo hayakubaliki, lakini leo kama yameingizwa rasmi katika sheria, tunataka tuone utekelezaji unafanyika Mhe. Mwenyekiti.

Tusione matangazo kama yale ambayo yapo yanapotosha watu kwamba kafanye kitendo hiki, ukimaliza unaweza kwenda kwa mganga wa kienyeji au kama tulivyokuwa tunayakuta pale ukaambiwa kwamba kuna dawa ya ukimwi, hakuna kitu kama hicho Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema maeneo mawili ya mwisho, hilo lilikuwa moja. La mwisho kabisa ni la kifungu cha 41 na 42 katika sehemu ya masharti mengineyo. Mhe. Mwenyekiti, hapa ninasisitiza kuwa kumetolewa haja ya serikali kusaidiana na jumuiya za watu wanaoishi au walioathirika na virusi vya ukimwi katika kupambana na ukimwi na vimetaja haja ya serikali kusaidia.

Mara nyingi katika bajeti mbali mbali tulipokuwa tukichangia Mhe. Mwenyekiti, kwamba mara nyengine kuna huduma ambazo serikali yenyewe haitoi kutokana na pengine uchache wa pesa au vitu vyengine. Sasa zile jumuiya ambazo zinatoa huduma hizi zinapaswa kusaidiwa na isiwe mapambano ya ukimwi yakawa ni miradi ya watu kujitengenezea fedha tu, lakini iende kwa walengwa.

Wakati fulani Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi tulikwenda kutembelea pale Chake Chake katika kukagua haya mambo ya vijana wanaotumia madawa ya kulevya. Tulikwenda pale, kuna kituo cha mambo ya ukimwi, lakini pia kinatoa huduma kwa vijana wanaotumia madawa ya kulevya.

Sasa kikaishiwa na fedha, wakasema wamewasiliana muda mrefu na serikali kusaidia baadhi ya vifaa tu pale Chake Chake ikashindikana. Lakini ukenda *ZAPHA+* Mhe. Mwenyekiti, kuna malalamiko kama haya. Sasa nilikuwa ninasema kwamba tumeona zipo kesi ambazo ninazijua Mhe. Mwenyekiti, za watu ambao wameathirika wamepatiwa dawa zile za kuwasaidia kuishi vizuri na unaona hali zao zinavyobadilika na wanaishi vizuri tu.
Mimi wapo watu ambao ninawajua hasa Mhe. Mwenyekiti, na ukimuona amebadilika hata huamini kama huyu ni muathirika, na hiyo ni tahadhari tosha kwa wananchi, usije ukaona mtu labda ukafikiria labda mpaka umuone mtu kadhofu dhofu, ukafikiri labda kaathirika na ukimwi, ukamuona mtu hali yake nzuri kabisa huku, wapo.

Kwa hivyo, ninasema wale wanaweza kuwa wanasaidiwa na serikali, lakini pia wanasaidiwa na jumuiaya kama hizi. Kwa hivyo, kuingiza kifungu kama hiki cha 41 Mhe. Mwenyekiti, ninadhani isiishie katika sheria, maana mara

nyingi huwa tunasema hapa tunakuwa wepesi mno wa kutunga sheria, lakini tatizo ni utekelezaji wa sheria.

Sasa ninadhani kwamba serikali imedhamiria kuzisaidia jumuiya hizi basi izisaidie kweli ili ziweze kutoa huduma hizi. Wale ndugu zetu walioathirika wanaishi katika mazingira magumu sana Mhe. Mwenyekiti.

Na Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia kifungu kabla sijakaa kitako, niseme lile ambalo nililisema punde. Hii ninaiambia serikali na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na ninamwambia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Kwanza wa Rais, aiangalie tena Tume yake ya Ukimwi.

Mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, nilikwamisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hapa kuhusiana na bajeti ya Tume ya Ukimwi, utaratibu wa demokrasia ambapo mimi ni muumini wake ambao ninauheshimu sana, walio wengi wakisema ipitishwe na utapitishwa na ilipitishwa. Lakini yale niliyoyasema na niliamini siku ile na ninaamini leo na nitaendelea kuyaamini kwamba kuna ubadhirifu mkubwa sana wa fedha katika Tume ya Ukimwi.

Labda fedha kutumika kupambana na ukimwi, badala ya fedha kutumika kusaidia walioathirika, fedha nyingi zinatumika katika makongamano na warsha ili kusaidia watumishi badala ya kusaidia walengwa waliokusudiwa. (*Makofi*).

Ninamuomba tena bajeti nyengine itakuja, sisi hatuchoki kusema ndio kazi yetu Mhe. Mwenyekiti, tunalipwa mishahara kwa kazi yetu hii ya kuja kusimamia maslahi ya wananchi, hatutochoka kusema. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri, bado ana miezi mengine 6 kabla ya bajeti yake haijamalizika, aitupie jicho Tume ya Ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninasema mswada ninaunga mkono, ninasisitiza tena kuna haja ya kuona utekelezaji wake uliokusudiwa unapatikana na tija iliyokusudiwa inawafikiwa walengwa.
Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi kusema machache kuhusu mswada huu na moja katika sababu kubwa ni kwamba Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais au wizara yake, kazi yake ni kukinga, sisi ikishatokea tunatakiwa tutibu. Kwa hivyo, kama kukinga tutaweza, maana yake sisi wenye matibabu tumepunguziwa kazi.

Kwa hivyo, sheria hii imekuja, kulikuwa na mambo mengi ambayo kama yanayosemwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu na wengine waliochangia, kwamba mambo mengi yalikuwa hata ukitaka kuyachukulia hatua unaweza ukaambiwa kwa sheria gani. Sasa sheria hii itatupa nafasi kufanya mambo mengine kuyafanya kwa utaratibu wa kisheria. Isipokuwa kuna mambo ambayo kwa kweli tunahitaji kushirikiana, sio sisi tu watu wa Serikali Kuu, lakini hata na serikali za mikoa, wilaya, shehia na hata Wawakilishi wenzetu waliomo katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa hivi sasa ambalo Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, wamejitahidi kushirikiana kujaribu kulikinga kwa nia hiyo hiyo ya kukingwa maambukizi. Lakini vita wanavyovipata unashangaa vinatoka wapi.

Jambo moja Mhe. Mwenyekiti, linalosababisha kuongezeka, jamii kukutana hasa vijana na umri wa vijana tunaujua, sisi wengine tena tunaanza kutoka. Lakini madisko, nyumba za starehe na ulevi umekuwa mwingi na hata utaratibu hazina. Ni mfano mzuri wa kutoa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, alipata malalamiko ya mwananchi Jambiani huko na Uroa, kwamba jamani eeh! yamezidi watoto wetu mpaka alfajiri hakuna *weekend* watu wana disko tu na humo ndio mambo hayo yanapofanyika. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo wakachukua hatua kushirikiana na wananchi, jamani tuzuwieni.

Kwa muda likafanikiwa, lakini *pressure* iliyotokea ni ya ajabu na ni ya miujiza, yaani kile kinachouwa raia wetu kinaonekana ndio kizuri, kile cha kutetea raia wetu kinaonekana kibaya.

Mhe. Mwenyekiti, sio vibaya ku-*declare some interest*, ni kwamba sisi wengine tunaishi katika maeneo ambayo majumba ya starehe yamezunguka, zamani ilikuwa hakuna. Lakini siku hizi hata humo tunamoishi munapigwa disko hazina muda. Maana tunafahamu Jumamosi na Jumapili kila mmoja na anachokipenda, lakini watu wafahamu kwamba ikifika saa 4:00 au 5:00 za usiku watu hulala, kuna wagonjwa, kuna watoto, kuna wale wengine ambao wanafanyakazi kwa kutegemea kesho wende wakazijibishe kwenye mawizara yao. Lakini saa 8:00 au 9:00 za usiku bado watu "hapana dawa" "hapana dawa" (hapa waziri wanaigiza kwa sauti ya kilevi), jamani nyinyi baada ya saa 1 au 2 swalaa. Kwa hivyo, ulikuwa unategemea ulale kidogo huwahi, baada ya muda mdogo unaitwa na Mwenyezi Mungu uende ukafanye wajibu wako.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo namshukuru, amechukua hima kwa hatua za kisheria, wengine amejaribu kuwanyang'anya

leseni, lakini bado anapigwa vita. Sasa unajiuliza tunapolalamika ukimwi aah, ukimwi hauzuiliwi na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji na Mhe. Juma Duni Haji. Ukimwi unazuiliwa na sote na kila linalosababisha kwamba lisitokee, basi sisi sote ni sehemu. Lakini wengine wanahisi kwamba kazi hii ni ya fulani na wengine wanapiga vita kwamba lisifanyike, matokeo yake ukimwi unaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, mfano tangu ukimwi kuanza mpaka sasa hapa Zanzibar karibu miaka 20 mpaka leo tunazungumza ukimwi, ukimwi eeeh! ndio sisi yaani ndio mimi na wewe unayesikiliza. Sasa kama unaongezeka, inaonekana kazi hii yetu sisi, ndio sisi jamii miaka 20. Ulifika hadi ukapungua, kuna maelezo ataeleza kitaalamu. Kuna *prevalence* na mambo mengine ya kuongezeka au kupungua. Ni sisi tunahitaji kila mmoja wetu awe sehemu ya hii.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ambalo wamezungumza mpaka Mhe Asha Bakari Makame na Mhe. Amina Iddi Mabrouk ni suala la madawa ya kulevya, yaani starehe, ulevi na zinaa ni kama mafya. Chungu hakikai kwenye jiko kwa mafya mawili, hata mguu ni lazima uzuilie hayo matatu, ndio uweze kusonga ugali. Sasa ukishalewa kama ni pombe au dawa ya kulevya, la pili unalotaka ni kucheza na ukishacheza la tatu tutaonana wapi. Sasa dawa ya kulevya inazidisha hivyo, lakini dawa ya kulevya vile vile watoto wanapigana sindano.

Kitu kimoja kinachotuathiri katika nchi hii na mimi nakiona na kinatuumiza hata sisi watendaji tulioingia serikalini ni muhali mkubwa. Mhe.Juma Duni Haji, unajua eeh! hapo nasikia panauzwa dawa. aka! sasa unaniambia mimi, nenda kaseme kunakohusika huyo akamatwe. Kila mmoja anaogopa.

Mhe. Mwenyekiti, utanisamehe kama muda bado upo kidogo dakika tano. Mimi na wizara yangu tunalaumiwa sana kuhusu watendaji wetu hawa wa Wizara ya Afya. Sijui ukenda hospitali kuna hivi na hivi, makelele kweli kweli. Nimeshasikia ilikuwa saa ngapi. Aah! nadhani ilikuwa saa 8:00 ile *shift* ya mchana. Je, unaweza kukumbuka nani alikuwepo pale, ulichukua jina. aah! maana yake sasa hilo nadhani wewe ungekwenda kulifuatilia. Hataki yeye awe lawamani, maisha anataka wewe uchukuwe hatua. Sasa sina ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina kesi kama mbili au tatu zilizokuwa watu wananilaumu, wakanipa ushahidi na tunazichukulia hatua. Lakini kila raia ana lalamika na ndio nchi nzima hii, tena sio sisi tu hata Tanzania Bara, waziri analalamika, Rais analalamika, Mheshimiwa, analalamika na askari analalamika. Muhali hatutaki kufanya yale yanayotustahikia. Kwa hivyo, madawa ya kulevya bado yanaendelea kuwepo, madawa ya kulevya ndio

yanayosababisha watoto wetu kuharibika na madawa ya kulevya ndio yanayoleta ukimwi.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda kule walipokuwa wale watoto walioathirika kufungua. Akaja mtoto wa kike mmoja akaeleza, kila mmoja alilia pale. Pale nikamnong'oneza mtu nikamwambia, wakishaondoka hapa basi wameshasahau hayo. Yaani yule mtoto anaeleza vile ilivyokua mpaka akaugua ukimwi, sote tulilia pale, kila mmoja alitoa kitambaa akafuta machozi. Lakini kushiriki yale yasitutokee hatutaki. Halafu nikaingia kule kwenye kile kijijumba chao nikawa natembea mule ndani, nikakuta maneno sijui kama nitaweza kuyakumbuka, lakini maneno yanasema hivi;

> "Binadamu ameubwa kupendwa, vitu vimeubwa kutumika, badala yake tunapenda vitu, tunawachukia binadamu"

Imeandikwa pale *slogan* nzuri kwa kizungu. Nikasema lahaula, sijui watu wanaifahamu maana yake hii, kwamba badala yakupendana binadamu tunapenda vitu, kila mmoja anatakiwa awe tajiri, tulivyotoka pale tumesahau. Hilo la pili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mahala hapa wajumbe walizungumza. Alizungumza Mhe. Mjumbe mmoja mambo ya ushauri nasaha na kwamba vituo vipo. Takriban vituo vyetu vyote siku hizi vinaruhusu kutoa ushauri nasaha. Lakini sio kila mtu anaruhusiwa kutoa ushauri nasaha. Ni lazima usomee na kuna taratibu zetu na watu wa kitengo chetu pale wanajua ufanye nini na nini na ufike daraja gani ndio unaweza ukatoa ushauri nasaha. Lakini vituo vipo vya kutosha vya kuweza watu kwenda wakapewa ushauri nasaha.

Kuna Mjumbe mmoja hapa alisema wanandoa wote wapimwe. Naona kama siku hizi ni kawaida. Mimi nimeshaziona harusi mbili hadi tatu zinazonihusu anachukuliwa ndugu yetu wa kiume anakwenda na mchumba wake kule, (*kudu kudu*) roho zinawapiga. Halafu wanarudi. Je, vipi aah! sote salama *Alhamdulillah*, halafu ndio ndoa inapita. Sasa hiyo iwe ni kitu cha kawaida, kisiwe ni kitu cha bahari mbaya, maana vile vile kuowa baada ya wiki mbili tena ukamkuta mwenzako yuko kwenye balaa, inakuwa sio nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, haya nadhani mawili au matatu ndio yatakuwa ya mwisho. Nilisema hapa mara moja na ninasema tena na kwa bahati nzuri wananchi wananisikia. Wengine wanalifanyia masihara wanasema ukimwi umekwenda pabaya, sijui asali imeingia sumu. Yote haya ni maelezo ya kutaka kuona kwamba jambo lenyewe ni gumu. Lakini mambo haya ni ya nafsi. Kila mara nikipata nafasi mimi husema kwamba hakuna kitu kigumu katika suala hili la ukimwi kama nafsi.

Nimeshatoa mfano na leo natoa mfano wala sioni tabu, kwamba sisi sote tuna ndoa, wale tuliokuwa na ndoa. Lakini Ramadhani inatuambia huwezi kula mchana na mama watoto unaweza kumwambia nisongee ugali ukaupiga ugali ukashiba ukafuta mdomo ukenda zako Msikitini kusikiliza darsa, anakujua nani kwamba umekula ugali. Mbona huli au hufanyi hivyo, kwa sababu nafsi yako unasema hili linanikataza.

Mhe. Mwenyekiti, hata tendo la ndoa kakuzuwia nani usikae na mkeo kwa tendo la ndoa mchana Ramadhani mbona hufanyi. Hufanyi kwa sababu nafsi yako inakuambia maadili yako kuwa hiki sistahiki kufanya. Waheshimiwa Wajumbe, hapa wamesema kuwa dini imetukataza kuwa "*la takrabu zinaa*". Ndio, Sasa mmoja anapokuambia bwana wewe, Mwenyezi Mungu keshakuambia usifanye, lakini kwa sababu nafsi yako huiwezi jikinge. Hoo! unatuletea makondom. akaa! usifanye umeshakatazwa na Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo, suala hili Mhe. Mwenyekiti ni la nafsi na nafsi ndio ngumu. Kwa hivyo, masheikh wetu waendelee kusema, lakini hili ni suala la mtu mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, suala la tatu ambalo nataka nilisema ni kuhusu mitandao, yaani *internet*. Sina uhakika kama kuna sheria hiyo labda Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, atawauliza watu wake au Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Mitandao yetu hii ya *Seltel, Tigo, Zantel* na mingine iko wazi, ninaposema kuwa ipo wazi ni kwamba wewe ingia *Google* sema chochote kinakuja, sasa haya mambo ya ngono ndio yanayowapelekea watoto wetu, anajua pale akishaandika kitu kadhaa na kadhaa, basi yanajaa madudu tele kwenye *screen*.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu waliokuwa katika njia ya kujikinga, ukenda mahotelini basi wanaeleza hasa kwamba unapofungua hii na hii inakuwa imefungwa, sasa hata kama utajaribu haiji kabisa. Wanakuambia kwa sababu ya x, y na z huwezi kuruhusiwa hii. Sasa kwa nini sisi hatufanyi hivi.

Kuna madudu Mhe. Mwenyekiti wee! mijidudu kweli kweli. Sasa sheria zetu au watu wetu Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, basi tushirikiane na watu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, iwe sio ruhusa hata ukipita pale iwe haiji, suala hili litatusaidia sana kwa sababu hamasa hizi nazo inategemea nini unachopenda, ukishakiona kwa macho matokeo yake unatafuta kutenda, balaa linazidi.

Mhe. Mwenyekiti, matangazo ameyasema Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Matangazo ya hapa nina dawa ya ukimwi au hapa ninatibu ukimwi. Suala hili tunaendelea kupambana nalo kama Wizara ya Afya. Kwa bahati mbaya ile

sheria ya afya *public health* mambo haya yote yamo, lakini utekelezaji wa ile sheria nikubwa. Kwa hivyo, imeshafika hatua lazima utangaze, Katibu Mtendaji lazima uwe na kamati hii na kamati hii, lakini tunakuja. Lakini vitu hivi haviruhusiwi mpaka uende kufanya usajili kwenye idara yetu kule ya madawa.

Sasa wengine hawataki kufanya hivyo na tunapowakataza na hasa Misikitini siku hizi kuna dawa zinaitwa dawa za kisuna. *Yarabbi* sijui dawa za sunna ni zipi, maana sunna unasema mwenyewe ina Mungu. Lakini nakuambia ni ugomvi Misikitini, tukiwaita kule Wizara ya Afya tukizungumza ni uhasama. Mtu akishapata maradhi, kwa nini hukunipa dawa. aa! wewe jamani dawa zote duniani hakuna isipokuwa dawa ya mkuyati.

Samahani Mhe. Mwenyekiti. Wanatangazia dawa za nguvu za kiume, eee! nguvu za kiume, hapa zinauzwa dawa za nguvu za kiume. Wanakwenda watu wanapata majidudu kisha wanakuja wizarani wamevurugikiwa, *system* haifanyikazi, bomba haiendi tena, maradhi ya *kidney*. Jamani haya yanatuathiri.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema niseme hayo kwa sababu naona yalikuwa nayo yanachangia katika matatizo. Sasa tunahitaji kushirikiana ili kulinda mambo haya na ninategemea sheria hii na sheria ile ya *Public Health* na kuna ile nyengine ya madawa ya kulevya, kama tutaacha muhali, basi tunaweza kupiga hatua kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, lakini muhali unatuumiza na viongozi wa maeneo, masheha na wa wilaya tushirikiane.

Sisi pale mtaani kwetu kwa upande ule kuna Gofu na halafu pale karibu kuna sijui *club* ile ya vijana hupigwa beni pale, basi ukiwa Dar es Salaam unalisikia saa 9:00 za usiku. Huku juu sijui kulikuwa na mwengine pale Raju. *Yaallah*, namuuliza sheha hivi mpaka saa ngapi hawa wanaruhusiwa, saa 6:00 za usiku au 7:00, kumbe saa 8:00 za usiku bwana, tena katikati ya wiki. Ninasikia pale kwa hawa jamaa ukenda wanakuwepo pale ni vijana wadogo, mimi sijawahi kwenda. Wengine huwa wananitania kuna watu huwa wanakwenda huko, ni vijana wadogo tu, jamii inakufa.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulipokuwa wadogo ule umri wetu, basi yakipita mazishi sisi tulikuwa haturuhusiwi kumuona maiti anapitishwa ile *Lailahailallah.* Siku hizi unamuona maiti kama vile kuku aliyechinjwa wala hakuna chochote na mambo yale mengine ya harusi. Samahani kina mama kwetu mwari havai kidani kama hajaolewa na hatii *lipstick*, umri wetu sisi ndivyo tulivyokuwa au sio Mhe. Asha Bakari Makame. *Lipstick*, kidani na hina mwanamwari wa Kitumbatu ilikuwa ni haramu. Loo! hivi sasa umkataze *Mashaallah* unaweza kupigwa mawe.

Kwa hivyo, kuna mambo ambayo ni ya msingi tunahitaji tushirikiane sote. Sio Waziri wa Makamu wa Kwanza na Waziri wa Afya tu, lawama hatuwezi kuacha kupokea maana ni wajibu wetu na tutakapokosolewa ndipo tutakapojua nini tumekosea. Lakini sio kila jambo sababu ni sisi.

Samahani Mhe. Mwenyekiti, nimalizie. Kuna wakati fulani angalau hivi sasa barabara zetu ni nzuri Waheshimiwa, wananchi nasema barabara zetu nzuri. Vijana Ijumaa jioni saa 2:30 au 3:00 usiku wanaelekea Mashariki huko, wanakwenda kufanya vitu vyao huko, wakirudi saa 8:00 za usiku chakaraa. Sasa gari inaendeshwaje. Anayeendesha gari mlevi, aliyepakiwa mlevi, mabio hayana kiasi na wanapata ajali katikati hapo. Wakishapata ajali mbio hospitali ya Mnazi Mmoja na daktari wetu mmoja keshawahi kupigwa pale hospitali.

Tena tumepeleka kesi Mahakamani, lakini ndio hayo hayo tunayosema. Basi wanataka lazima mgonjwa wao atizamwe mwanzo, ee bwana wee. Kuna watu wametangulia mwanzo, lazima wahudumiwe wao, wakampiga daktari wetu. Sasa nauliza hivi kakuambia nani ukalewe upate ajali. Inakuwa ni lawama ya kwetu sisi tu daktari kutibu, lakini wewe mwenyewe kujilinda huwezi.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kuchangia hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya na wewe kwa mchango wako wa hoja ambayo tuliyonayo mbele yetu. Waheshimiwa Wajumbe, kwa muda uliobakia sifikiri kama utamtosha Mhe. Waziri, kuja na yeye kufanya majumuisho. Kwa hivyo, nichukuwe fursa hii kuwashukuru sana kwa wale ambao wametoa michango, lakini na kwa wengine ambao hawajatoa michango, basi niwashukuru kwa utulivu wao.

Mhe. Waziri, atafanya majumuisho jioni. Kwa hivyo, ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe tufike mapema ili tuweze kupata majibu kwa maswali ambayo tumeyauliza. Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe.

(Saa 6:44 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa taarifa niliyoipata kutoka kwa Mwenyekiti aliyekuwa akiongoza kikao hichi asubuhi wachangiaji walikuwa wamemalizika na sasa ni nafasi ya Mhe. Waziri, ili apate nafasi ya

kufanya majumuisho na kujibu baadhi ya hoja na baadae tuweze kupitisha Mswada huu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kuweza kukutana tukiwa wazima na wenye afya kwa lengo la kuendelea na shughuli zetu za kuwatumikia wananchi.

Nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kutoa majibu na baadhi ya ufafanuzi juu ya michangio mbali mbali iliyotolewa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika kuujadili Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya Ukimwi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Mwenyekiti, na Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kuweza kuupitia Mswada huu kwa kina na kuweza kuufanyia marekebisho muhimu ili kuufanya uwe bora zaidi. Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba uniruhusu kuwataja Wajumbe waliopata fursa ya kuchangia Mswada huu kwa kuzungumza ndani ya Baraza lako tukufu, lakini pia waliochangia kwa maandishi:

1) Mhe. Mwenyekiti wa Kamati kupitia hotuba yake iliyowasilishwa kwa niaba yake na Mhe. Shadya Mohamed Suleiman wa Viti Maalum.
2) Mhe. Salma Mohammed Ali
3) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
4) Mhe. Hamza Hassan Juma
5) Mhe. Mgeni Hassan Juma
6) Mhe. Panya Ali Abdalla
7) Mhe. Saleh Nassor Juma
8) Mhe. Wanu Hafidh Ameir
9) Mhe. Salim Abdalla Hamad
10) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
11) Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
12) Mhe. Abdalla Mohamed Ali
13) Mhe. Hassan Hamad Omar
14) Mhe. Abdi Mossi Kombo
15) Mhe. Amina Iddi Mabrouk
16) Mhe. Asha Bakari Makame
17) Mhe. Ismail Jussa Ladhu

18) Mhe. Juma Duni Haji (Waziri wa Afya)

Waliochangia kwa maandishi ni:

19) Mhe. Suleiman Hemed Khamis
20) Mhe. Marina Joel Thomas

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu umepata bahati ya kuchangiwa na Wajumbe wapatao 20. Sasa naomba kwa idhini yako kutoa baadhi ya ufafanuzi. Nitaomba pale ambapo nitakuwa sijajibu basi sio kwa makusudi lakini tu labda tutawekana sawa katika vifungu, lakini tutakuwa tumejitahidi. Pia, sitomjibu Mwakilishi mmoja mmoja, lakini nitakusanya zile hoja ambazo zimewakutanisha wengi na kuzijibu kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, suala ambalo lilitawala sana ni juu ya tafsiri ya mtu aliyeathirika. Hichi ni kifungu cha 2. Wachangiaji wengi waliona kwamba kifungu hiki kinawajumuisha watu ambao hawana UKIMWI pamoja na watu wenye ukimwi. Lakini kwa mujibu wa tafsiri ambayo inatumika na labda tukiyatumia maneno ya Kiingereza tutaweza kufahamu zaidi nini kilichokusudiwa. Maana ya neno mtu aliyeathirika usawa wa neno lake la kizungu na *affected person;* mtu ambaye ameathirika kwa kiasi fulani kwa njia moja au kwa njia nyengine.

Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI hawa wao sio waathirika ni tofauti na waathirika, lakini wao kwa kizungu labda neno zuri la kutumia ni *infected person;* hawa ni watu ambao wao wanavyo virusi vya ukimwi. Kwa kawaida hatuwaiti waathirika tunawaita watu wanaoishi na virusi vya ukimwi, hiyo ndiyo tofauti.

Mtazamo wa mtu aliyegundulika na virusi vya ukimwi nimeitoa hiyo tafsiri, lakini Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Mgeni Hassan Juma, waliweza kueleza ufafanuzi huo kwa kina takriban wananchi wote Watanzania na Wazanzibari ni waathirika wa janga hili la Ukimwi kwa njia moja au nyengine. Aidha ndani ya familia yako au watu unaofanya kazi nao au wenye mahusiano nao, wao ni watu ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI. Kwa kuwa wao wako hivyo wewe mwenyewe sehemu ya nafsi yako nayo inakuwa imeathirika kwa njia moja au nyengine. Hiyo ndio maana ambayo tumeikusudia hapa. Nawashukuru sana Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Hamza Hassan Juma; Mwenyekiti wangu wa Kamati nao walisaidia kutoa ufafanuzi.

Tunaposema waathirika kitaifa ndio zaidi sasa maana wafanyakazi, vijana ambao wao ndio wengi waathirika na ndio watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI basi taifa linaathirika kwa nguvu kazi yake kuweza kuwa nyingi

nayo imo katika maradhi haya ya UKIMWI. Hayo yalizungumzwa sana juu ya kupata ufafanuzi huo na Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Mhe. Amina Iddi Mabrouk.

Lakini neno la pili ambalo nalo lilitakiwa ufafanuzi lakini si ufafanuzi hasa lakini liliulizwa na Mhe. Abdalla Juma Abdalla na Mhe. Wanu Hafidh Ameir, ni tafsiri ya neno ulemavu. Zilikuwepo mbili pale nikaulizwa Mhe. Waziri, ipi hasa iliyokusudiwa. Nasikitika kuomba radhi kwamba Mswada wetu tuliwasilisha na rundo la marekebisho ni mengi na pengine muda umekuwa mfupi, Wajumbe hawakupata muda wa kupitia, kwa kweli ile ilikuwa tayari imeshafanyiwa marekebisho na ukiangalia *schedule of amendment* iliyowasilishwa leo katika kifungu cha 7 kinasema kwamba inayotumika kama maana ya ulemavu ni ile iliyokuwepo kwenye *paragraph* ya pili.

Vile vile, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, alitaka ufafanuzi juu ya huduma za afya na akasema vile ilivyo haieleweki. Naomba kumuarifu nayo pia ilikuwa tayari imefanyiwa marekebisho katika *items* ya 11 katika jaduweli la marekebisho. Pia, alitaka kujua juu ya kifungu cha 5(2) (b) kwamba tunamaanisha nini, je ni kwa hiyari tunaposema mtu ana wajibu wa kujua afya yake na akasema labda tutumie neno kulazimisha. Wajibu anavyofahamu yeye ni kulazimisha. Sisi tunasema kwamba kupima virusi vya UKIMWI ni suala la hiyari sio la kulazimisha, lakini akasema mbona tunatumia neno wajibu.

Kwa kweli sijui labda Kiswahili hatujapata neno zuri zaidi la kutumia. Wajibu huu ni kwamba mtu mwenyewe halazimiki kwamba ni lazima apime. Isipokuwa ni wajibu wake aweze kujua afya yake, hicho ndicho kilichokusudiwa lakini sio kulazimisha.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla, pia, alizungumzia mgongano uliopo katika kifungu cha 12(3) na 12(4) vifungu hivi kwa kweli havina mgongano labda jinsi yeye tu alivyovisoma na kuvifahamu, lakini vipo sawa sawa. Moja kinalinda haki ya usiri wa mtu ambaye amechunguzwa, lakini cha pili kinampa *right* yule ambaye anaweza kuingizwa damu au viungo kuweza kujua kwamba kile anachoingiziwa hakina madhara yoyote.

Mhe. Salma Mohammed Ali, kidogo alitaka tumueleze vipi tutausoma ukimwi kwa *capital letters* kwa sababu kwenye *schedule of amendment* imeandikwa lisomeke kwa herufi kubwa. Nafikiri ni mazoea tu, tumezoea kutumia hili neno lakini lilokusudiwa liandikwe kwa herufi kubwa likimaanishwa kwamba lile neno UKIMWI ni *abbreviation* ni Ukosefu wa Kinga Mwilini, sio kwamba kulisoma kwa *capital letters*.

Mhe. Mwenyekiti, akiwemo Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Bikame Yussuf Hamad na Mhe. Wanu Hafidh Ameir, walizungumzia suala la ulazima wa wanandoa nao kwamba wapime afya zao kabla ya kufunga ndoa. Tayari kwenye Mswada huu na siku zote tunasisitiza kusema kwamba upimaji wa virusi vya UKIMWI ni suala la hiari. Sheria inakataza kwamba mtu asilazimishwe isipokuwa pale tulipotaja yale makundi ambayo tumeyataja kwa kuyaeleza. Kwa kweli haikatazwi watu wenye virusi vya ukimwi kuoa au kuolewa na mtu ambaye yeye yupo huru hana virusi vya ukimwi.

Mazoea ambayo tumejiwekea na ni mfumo mzuri tuliojiwekea kwamba utaratibu wa wanandoa kwenda kupima ni kufahamu afya zao ili kuweza kujua ndani ya ndoa wataendeleaje. Haikuletwa kwa maana kwamba mtu akigundulikana ana virusi basi huyo hafai kuoa wala kuolewa. Hivi leo ndani ya jamii yetu kuna watu ambao wana virusi na wanaishi na virusi vya UKIMWI, lakini wenza wao hawana virusi hivi, hilo hatukuona kwamba linaweza kuingizwa pale kwa sababu ni suala la hiari. Hata hivyo, tunasisitiza kwamba elimu hii ya wenza kuweza kujua afya zao, ni muhimu iendelezwe kama inavyoendelea hivi sasa.

Mhe. Salma Mohamed Ali, alisema kwa nini basi tumeweka wajawazito hapa. Madhumuni na lengo la kuwapima wajawazito ni kuweza kumuhifadhi kiumbe ambaye yumo ndani ya tumbo la mama. Tunajua kwamba kuna utaalamu sasa hivi wa kuweza kumuhifadhi mtoto ambaye anazaliwa na mtu anayeishi na virusi vya UKIMWI, lakini mtoto akazaliwa akiwa yupo huru. Lakini ikiwa hujajua afya ya mama inawezekana kama mama yule hajapimwa mama mwenye UKIMWI akaweza kumuambukiza kiumbe ambacho atakizaa akazaa mtoto mwenye UKIMWI. Kwa hivyo, hiyo ndio maana akina mama wajawazito tukawa tumewaweka kwenye *category* kwamba wao wapimwe UKIMWI.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Salma Mohamed Ali, pia walizungumzia suala la vyuo vya mafunzo na jinsi gani sheria hii itaweza utekelezaji wake kuweza kuzingatiwa sawa sawa na mazingira yenyewe yalivyo. Kwa kweli tunafanya kazi kwa karibu sana na Wizara husika na ofisi yetu kupitia Tume imeandaa mkakati na kupambana na mazingira hatarishi, na tayari umeanza kutekelezwa kwa ajili ya kuweka mazingira ya kuweza kurahisisha utekelezaji wa sheria hiyo. Mashirikiano katika utekelezaji wa sheria hii ni ya taasisi nyingi tukiwemo sisi wote wanajamii.

Katika kifungu cha 4(a) Mhe. Abdalla Juma Abdalla, alihoji kwamba kuna ulazima wa mtu kupima virusi kwa suala la hiari. Tunaendelea kusema tena kwamba mtu ana wajibu wa kupima. Hili nimeshalitolea maelezo ya kutosha.

Katika kifungu (a) na (b) Mhe. Panya Ali Abdalla, alizungumzia juu ya suala la elimu katika mapambano yetu, lakini akasisitiza kwamba elimu hata ikitolewa kiasi gani ni lazima na sisi wenyewe tuweze kubadilika, jamii ibadilike na sisi tunakubaliana naye moja kwa moja. Tunaiasa jamii kwamba elimu tunayopewa ni lazima sisi wenyewe tuweze kubadilika ili iwe na mafanikio katika kutukinga katika janga hili la UKIMWI.

Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Salma Mohamed Ali, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, alizungumzia suala la elimu hii kutolewa katika vyuo vya Madrasa kutokana na wimbi la udhalilishwaji wa watoto unaofanywa na baadhi ya walimu wa Madrasa. Hili tunalikubali na tayari tumeshaanza kulifanyia kazi kwa kushirikiana na Jumuia ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA).

Mhe. Panya Ali Abdalla, alitaka kujua Waziri atamruhusu mfanyakazi atakayetoa huduma za upimaji, kwani wakati mwengine Waziri atakuwa hayupo na mambo kama hayo. Hii ni kwamba Waziri ndiye anakuwa dhamana, lakini Waziri ana watu wake wengi ambao wanaweza kufanya shughuli hiyo.

Katika kifungu cha 27, Mhe. Salim Abdalla Hamad, alitaka kupigiwa marufuku watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kuingia Zanzibar. Kuna haja ya kuiangalia hali hii kwa upana zaidi, tukiweka marufuku ya watu wenye Virusi vya UKIMWI kuja kwetu, je, wale wetu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI nao wasiruhusiwe kutoka nje kwenda katika maeneo mengine. Na je, wale wetu wanaotaka kurudi kwao nao wasiruhusiwe. Tusiliangalie kwamba suala hili ni la wageni tu kwamba ndio wanaoleta UKIMWI, lakini humu ndani ya jamii yetu basi uenezwaji na maambukizi ya Ukimwi haya yanaweza kuwa yanatokea kwa kiwango kikubwa.

Namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hamza Hassan Juma, yeye kwa kweli alitoa elimu kubwa katika suala zima la kuepukana na unyanyapaa ndani ya jamii yetu. Namshukuru sana, yeye tulifanya kazi naye kwenye Kamati kwa pamoja katika Mswada huu na ametusaidia katika kufanya marekebisho makubwa sana ndani ya masuala haya na amewaasa wananchi juu ya njia bora za kuweza kuondokana na unyanyapaa, lakini vile vile juu ya suala zima la kuondokana na maambukizi ya UKIMWI.

Mhe. Mgeni Hassan Juma, yeye alitoa ufafanuzi zaidi wa mtu aliyeathirika, lakini vile vile alikuwa ana uelewa mpana wa masuala haya na alitusaidia sana katika kuelimisha jamii yetu. Lakini vile vile, alitahadharisha kwamba elimu itakayotolewa katika makundi maalumu izingatie mila, silka na tamaduni zetu. Na sisi tunalikubali hilo kwamba hatutoiga tu nchi fulani ya

kigeni inafanya hivi na mambo yale yapo kinyume na maadili yetu na sisi tukayaleta kwetu. Elimu yoyote itakayotolewa na Tume itazingatia silka, mila na tamaduni zetu.

Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Saleh Nassor Juma, wamegusia sana na wao suala la kuwepo kwa vichocheo na vishawishi vya kuongeza UKIMWI. Mhe. Saleh Nassor Juma, aliendelea kutaja hata mavazi ya vimini, mavazi ambayo alieleza kisayansi kwamba yanachochea watu kufanya tendo la kujamiiana.

Lakini tunataka kueleza kwamba katika nchi hii vimini ni marufuku. Kuna sheria ambayo imewekwa mwaka 1972 ya kulinda utamaduni na silka ya Mzanzibari imepiga marufuku uvaaji wa vimini na nguo nyengine ambazo haziendani na silka na tamaduni za nchi yetu. Lakini ni usimamizi tu wa sheria yenyewe. Kwa hiyo, anapoona watu kama hao wapo katika mavazi ambayo yanashawishi ni vyema akachukua hatua yeye kama mwananchi ili kuweza kuyashughulikia hayo yakawa vizuri zaidi. Hiyo, ilikuwa kwenye suala zima la mavazi ambayo yanachochea hasa katika suala la vimini.

Lakini vile vile, nimueleze Mhe. Waziri wa Afya alitueleza vizuri kwamba mambo mengi na vishawishi vingi vipo lakini kinachotakiwa hapa ni kupigana na nafsi yako, kusema kwamba hili limekatazwa na hili sitolifanya. Kwa hivyo, yote hayo mawili ni ya kuzingatia kwa pamoja.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Suleiman Hemed Khamis, walizungumzia suala zima kwamba hawa watu wenye Virusi vya UKIMWI watangazwe, wasifichwe pasiwepo na usiri.

Napenda tu kutoa taarifa kwamba tunapowatangazia watu hawa kwanza ni lile suala la unyanyapaa ambalo tunatakiwa tulipige vita. Lakini hilo linaweza kutusababishia kwamba mtu anayejihisi ana virusi vya ukimwi hatokwenda tena kupima na itabaki maambukizi yapo makubwa ndani ya jamii yetu kwa sababu watu hawajui *status* ya afya zao.

Lakini vile vile, ilitoka *suggestion* kwa baadhi ya Wajumbe akiwemo Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Asha Bakari Makame, Mhe. Abdalla Juma Abdalla, kwamba kwa nini watu hawa wasishtakiwe. Watu ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI na kwa makusudi wakaambukiza watu wengine ambao wao walikuwa hawana virusi vya UKIMWI. Katika sheria hii hakuna kipengele kinachowabana kwa sababu tayari kwenye Sheria ya Makosa ya Kujamiiana suala hilo limezingatiwa, hasa katika suala zima la mtu yeyote kuweza kumuambukiza maradhi mtu mwengine kwa makusudi basi nalo gonjwa la UKIMWI linaingia hapo.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad, na Waheshimiwa wengine waligusia suala la kwamba tunaonekana tumewabeba sana watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kuwatetea mno watu hawa si malaika na wao wanafanya makosa. Sheria hii haikatazi mtu ambaye anaishi na Virusi vya UKIMWI kushtakiwa kwa makosa ambayo atayafanya, yeye ni sawa sawa na mwananchi mwengine, haikatazi hilo. Kwa hivyo, hatuwaweki wao kama malaika, ni watu ambao wanaishi katika jamii kama wengine na wanaweza kushtakiwa kama wengine.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alizungumzia suala zima katika kifungu cha masuala yanayohusiana na haki za binaadamu kwamba kwa nini tumechukua *item* moja tu pale lakini kuna sura nzima ambayo inazungumzia suala hilo. Kwa kweli na hilo nalo tumekuwa tumeshalirekebisha katika *item* ya 15 ya jaduweli ya marekebisho na sasa sura ya tatu nzima imezingatiwa ya Katiba yetu katika kuzingatia haki za binaadamu.

Kuhusu maoni pia ya baadhi ya Wajumbe kwamba Mswada huu labda umeangalia zaidi kuwalinda watu wanaoishi na Virusi, tuusome vizuri huu Mswada. Mswada huu unawahusu wanaoishi na Virusi na wengine wote walioathirika. Kwa maana ambayo nimeitoa hapa ya waathirika ina maana Mswada huu unatulinda sote. Ndio maana kuna yale mambo yanayohusisha mtu kuweza kujua afya yake, mtu kuweza kupata huduma zinazostahiki na mambo kama hayo. Kwa hiyo, haujawaacha watu ambao hawaishi na Virusi vya UKIMWI, umewahusisha watu wote.

Mhe. Asha Bakari Makame, amezungumza sana kuhusiana na suala zima la unyanyasaji wa watoto, lakini pia sasa hivi tabia mbaya imeingia hata kwa watu wazima vile vile. Watoto wetu wa kiume na wanaume kwa unyanyasaji wa kijinsia na alisema hapa lazima tuchukue hatua muafaka. Nakubaliana naye, masuala haya ni mengi na yanasababisha maambukizi ya UKIMWI.

Kwa hiyo, kama jamii sote tunahusika katika kulitafakari hili na kuona jinsi gani linaondoka ndani ya jamii yetu. Hapo awali hatukuwa na suala hili ndani ya jamii yetu. Hata kama lilikuwepo halikuwa katika kiwango hiki. Ni juu yetu tujue ni sababu gani zinazosababisha, kama zipo sababu zinaweza kuondoka, lakini pia kuwachukulia hatua kali wanaohusika na masuala yale ili kuyakomesha ndani ya jamii yetu.

Namshukuru sana Mhe. Amina Iddi Mabrouk, naye alitoa elimu ya aina yake na kuwataka na kuwahamasisha sana wananchi wetu juu ya kutoogopa kwenda kujua afya zao katika suala zima la kupima Virusi vya UKIMWI. Tunashukuru sana tukipata watu kama hawa ambao wanaweza kuhamasisha

jamii kwa sababu wanaweza kutusaidia. Pia, alizungumzia suala la kuwaondoa wafanyakazi ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI katika sehemu wanazofanya kazi na kuwa wawekwe katika sehemu ambazo zitakuwa salama kwa afya yao. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, hilo limezingatiwa katika kifungu cha 25(3) cha Sheria yetu hii au Mswada ambao tumeuleta mbele yetu.

Wajumbe wengi akiwemo Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Amina Iddi Mabrouk na wengine walizungumzia uhusiano wa karibu uliopo juu ya matumizi ya dawa za kulevya hasa kwa kujidunga sindano na maambukizi ya UKIMWI. Hili ni kweli na sisi wenyewe katika takwimu zetu tumeliona kwamba maambukizi kwa watu wanaotumia dawa za kulevya hasa kwa kujidunga sindano ni makubwa zaidi kuliko kwenye makundi mengine. Kwa hivyo, ni wajibu wetu sote kwa pamoja kuyapiga vita na kushirikiana katika vita vigumu vya kupigana juu ya mapambano haya ya dawa za kulevya, hili ni jukumu letu sote, kwa hiyo tunahitaji kulifanyia kazi.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk, alituasa tusitumie neno mila potofu katika Mswada huu, lakini ningemuomba aangalie *item* ya 10 katika marekebisho ya Mswada au aiangalie tafsiri yenyewe tunakusudia nini kwa mila potofu. Ni zile mila, tabia, desturi ambazo zinahatarisha afya za watu au kuharibu mazingira ya watu ambao wanaishi kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wako wengi akiwemo Mhe. Abdi Mossi Kombo, Mhe. Bikame Yusuf Hamad, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Hamza Hassan Juma, wote walisisitiza kwamba bado tunahitaji elimu itolewe kwa wingi, lakini kuna waliosisitiza kwamba kuna makundi maalum, mfano wa watu ambao wako dago na waliopo katika *remote areas (rural areas)* Mhe. Bikame Yussuf Hamad, alieleza haya kwamba labda elimu hii haiwafikii.

Kipindi cha nyuma sana yale ambayo ameyazungumza ndiyo yaliyokuwa yakitokea hasa ndani ya jimbo lake, sinema za bure zilikuwa zinaoneshwa huko, lakini kidogo kutokana na bajeti iliyokuwa ikitumika kwa shughuli zile kumalizika utaratibu ule umeondoka, lakini hili tumelifanyia kazi. Madhumuni yetu ni kwamba jamii yote bila ya kujali chombo gani kitatumika wapate elimu juu ya kujikinga na maambukizi ya janga hilo la UKIMWI.

Kwa hivyo, hilo tunalichukua na elimu itaendelea kutolewa siku hadi siku.Mhe. Saleh Nassor Juma, alitaka kujua kwa nini hatuna kipengele kinachowataja wanaume. Tulipozungumzia kifungu cha 33(1) wanaume na wavulana lakini tumeandika wanawake na wasichana. Mswada huu unawalinda watu wote kama nilivyoanza kusema lakini hawa wengine

wametajwa mahsusi kutokana na mazingira yao hatarishi. Kwa hivyo, ndio maana wakatajwa hapa. Lakini kwa jumla nao wanaume na wavulana wamo katika kulindwa ndani ya sheria hii.

Mhe. Saleh Nassor Juma, alizungumzia suala zima la kuwepo na mabaa karibu na makaazi na skuli. Namuarifu Mheshimiwa kwamba sheria ipo na Mahkama ya Vileo ipo, wananchi wanapoona wakati wowote kwamba kuna sehemu ya vileo karibu na makaazi yao wanayo haki ya kupinga kuwepo kwake. Kwa hivyo, afanye tu utaratibu wa kulielewa hili zaidi ili kuona kwamba wanafunzi wetu hawaathiriki.

Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabla sijamaliza Mhe. Suleiman Hemed Khamis, ambaye na yeye alikuwa na maswali ya ziada. Ametuasa kwamba sheria hii ikishawekwa saini tu tuharakishe kutengeneza Kanuni kwa sababu mara nyingi serikali tunachelewa kutengeneza kanuni ambazo zinawezesha urahisi wa kutekeleza sheria hii. Namuahidi kwamba tutafanya hivyo sheria hii ikishawekwa saini.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis, alitaka kujua kwamba serikali inafanya nini katika kufahamu jitihada za kupata za maambukizi ya ukimwi kwa vijana wenye umri mdogo. Takwimu hizo zipo, zinapatikana kupitia kitengo cha kudhibiti UKIMWI.

Pia, aliuliza, je, ni msaada gani unaotolewa kwa vijana hao badala ya kugundulikana kwa vijana hao hupewa rufaa na kupelekwa katika vituo vya tiba kwa uchunguzi zaidi. Wanaohitaji matibabu huanzishiwa dawa, halafu wanaunganishwa na vijana wenzao katika maisha ya *ZAPHA+* na wanapewa elimu rika, wanapatiwa *study* za maisha na wanapatiwa baadhi ya misaada ikiwemo mambo yao ya kuweza kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa, ameniuliza ni mara ngapi nimetembelea *Sober House* niseme ni mara kadhaa kwa ghafla hizi siwezi kujua *data* lakini nyingi zao karibu zote nimeweza kuzitembelea kama zipo ambazo nitakuwa sijazitembelea zitakuwa ni hizi ambazo zimeanzishwa karibuni na alitaka kujua zipo ngapi. *Sober House* kwa sasa zipo 14, zilizopo Unguja ni 9, na 5 zipo Pemba na alitaka kujua zipo zinazokuja mpya? Katika hizi 5 za Pemba, 2 ni mpya, 1 ipo Mbuyuni Mkoani Pemba na ya pili ipo Mtukitu Chakechake.

Mheshimiwa, tunapokea ushauri wako na kuunga mkono juhudi za wana *Sober House*. Pia, alitaka kujua kuna juhudi gani za kuwafichua walioathirika, hili tayari nimeshalijibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sasa naomba kutoa hoja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Sasa tuwahoji ndugu Wajumbe wale wanaokubaliana na Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Kukinga na Kusimamia Masuala ya UKIMWI Zanzibar, Kulinda na Kuendeleza Haki za Watu Wanaoishi au Walioathirika na Virusi vya UKIMWI na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo wanyooshe mkono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe
)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Masharti ya Kukinga na Kusimamia masuala ya Ukimwi Zanzibar ya 2013

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	Jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.
Kifungu 2	Tafsiri pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Pili

Majukumu ya Ujumla

Kifungu 3	Wajibu wa jumla wa Tume pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 4	Wajibu wa jumla wa watu pamoja na marekibisho yake.

Sehemu ya Tatu

Taarifa, Elimu na Mawasiliano kuhusu Virusi vya Ukimwi na Ukimwi

Kifungu 5	Taarifa na Elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 6	Elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi katika Taasisi za Elimu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 7	Taarifa na Elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi kama huduma ya Afya pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 8	Taarifa na Elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi katika sehemu za Kazi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 9	Taarifa na Elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi na Vyombo vya Habari pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 10	Taarifa na Elimu ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi katika jamii pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne

Utaratibu, Matendo na Hatua za Kujikinga na Virusi vya Ukimwi na Ukimwi

Kifungu 11	Hatua za Kinga pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 12	Kuvifanyia vipimo viungo vya mwili vilivyotolewa mchango pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 13	Kinga ya Maambukizi Kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 14	Miongozo wakati wa Upasuaji na Taratibu zinazofanana pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tano

Ushauri na Kupima Virusi vya Ukimwi na Ukimwi

Kifungu 15	Ushauri Kabla na Baada ya Kupima Virusi vya Ukimwi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 16	Mambo ya Kuzingatiwa wakati wa Kutoa Ushauri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 17	Mambo ya Kushauri baada ya Kupima.
Kifungu 18	Kupima Virusi vya Ukimwi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 19	Masharti ya Kituo cha Kupima pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 20	Kukataza kupima kwa Lazima pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 21	Ridhaa ya Kupima Ukimwi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 22	Matokeo ya Kupima Virusi vya Ukimwi pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Sita

Ulinzi wa jumla wa Haki za Mtu anayeishi au aliyeathirika na Virusi vya Ukimwi

Kifungu 23	Katazo la Jumla la Ubaguzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 24	Usiri na Ufichaji wa Hali ya Ukimwi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 25	Ubaguzi katika Uajiri pamoja na Marekebisho yake.

Kifungu 26 Ubaguzi katika Taasisi za Elimu pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 27 Kizuizi kwa Kusafiri na Makaazi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 28 Kuzuiwa katika Utumishi wa umma pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 29 Kuondolewa katika huduma ya Mikopo na Bima pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 30 Ubaguzi katika Taasisi za Afya pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 31 Upatikanaji wa Huduma za Afya pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Saba

Kulindwa kwa Makundi Hatarishi na Watu waliokuwa katika hali ya Hatari zaidi

Kifungu 32 Watoto wanaoishi au waliathirika na Virusi vya Ukimwi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 33 Ulinzi wa Wanawake na Wasichana.

Kifungu 34 Watu wenye Ulemavu pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 35 Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nane

Ukimwi na Virusi vya Ukimwi Vinavyohusiana na Utafiti wa kibinaadamu

Kifungu 36 Utafiti na Majaribio ya Tiba pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 37 Ridhaa ya Utafiti pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tisa

Makosa Mengine yanayohusiana na Virusi vya Ukimwi na Ukimwi

Kifungu 38 Makosa yanayohusiana na Kuvujisha Siri.

Kifungu 39 Taarifa za Kupotosha.

Kifungu 40 Makosa yanayohusiana na kuharibu pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Kumi

Masharti Mengineyo

Kifungu 41 Kusaidia Jumuiya za Watu wanaoishi au walioathirika na Ukimwi pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 42 Kusaidia Jumuiya za Watoa huduma majumbani pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 43 Adhabu ya Jumla pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 44 Masharti ya Jumla kuhusiana na Adhabu pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 45 Kanuni pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 46 Kupingana na Sheria nyengine.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mkono, wanaokata, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Masharti ya Kutunga na Kusimamia masuala ya Ukimwi Zanzibar ya 2013

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa mswada wa Sheria ya Kukinga na Kusimamia mambo ya Ukimwi Zanzibar ya 2013 usomwe kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri, wanyanyue mkono, wanaokata, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kumalizika kwa kazi hii nzito na muhimu sana kwa siku ya leo na kazi inayotukabili mbele yetu ni uwasilishaji wa ripoti ya Kamati Teule, ripoti ambayo ni kubwa na itatumia zaidi ya masaa matatu katika uwasilishaji wake. Kwa hivyo, basi nafikiri ingelikuwa jambo la busara, ripoti ile tukaiwasilisha hapa kesho asubuhi na mapema baada ya kipindi cha maswali na majibu, lakini kwa sasa kabla ya hatujaakhirisha Baraza letu nimuombe Mhe. Mwanasheria atusaidie hapa, kuna taarifa tumeletewa hapa ya kuhuzunisha.

Kuna vijana wetu kutoka *SUZA* wamepata ajali Dodoma wakitokea kwenye michezo, vijana 16 wamepata maumivu madogo madogo na wamesharuhusiwa, lakini vijana wawili wamepata maumivu makubwa na wamelazwa *ICU* na hatujapata habari zaidi. Taarifa hii imewasilishwa na Mhe. Ali Juma Shamuhuna, ili tuweze kujulishana sote tupate kuelewa tatizo ambalo limejitokeza muda mfupi uliopita.

Kwa msingi huo basi naomba nimkaribishe Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu ili atusaidie katika taratibu za kisheria tuweze kuliakhirisha Baraza letu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile shughuli zilizopangwa katika orodha ya shughuli za leo hazijakamilika, lakini pia kwa vile muda uliobaki hautotosha kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liridhie kuakhirisha kabla ya muda wake ili tuweze kukamilisha shughuli hiyo kesho asubuhi.

Naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa mara nyengine tena nachukua fursa hii kuwashukuruni na vile vile kuliakhirisha Baraza hili hadi kesho siku ya Jumanne tarehe 17/12/2013 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 11.47 Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 17/12/2013 saa 3.00 asubuhi)